tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



**Vitambi** vya polisi vyamshtua Samia, ahadharisha lijalo

UKURASA 2


Ukurasa 12
Jengo jipya Umoja Posta Afrika linavyoakisi mabadiliko kidijitali
Ukurasa 13
Midahalo waathirika ukatili ilivyo mwalimu bora kukabili wanyanyasaji
Nipashe TESA
Jumanne Septemba 5, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Ukurasa 14
Ndivyo wachafuzi wakubwa mazingira kama hawa wanavyoendelea kuitesa Afrika
ELIMU
NA MARCO MADUHU, SHINYANGA
Mtaalamu atoboa siri kubomoka familia, utandawazi kunavyoumiza malezi, makuzi
• Kila saa moja ndoa 13 huingia migogoro, balaa kasi ya talaka
KUNA usemi kuwa samaki akunjwe angali mbichi, ukimaanisha kwamba mtoto anatakiwa kufundishwa vitu vingi kuanzia mwenendo mwema, maadili na elimu ya dunia akiwa mdogo si baada ya hapo.
Mtoto akifundishwa jambo akiwa mdogo ni rahisi kulishika na kulifanyia kazi lakini pia atakuwa na kumbukumbu kila anapoona anakwenda tofauti na maelekezo ya kile alichofundishwa na mlezi au mzazi na hata mwalimu.
Annastazia Rugaba ni Meneja Utetezi kutoka shirika la TWAWEZA, anayewakumbusha wazazi na walezi kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia na kuachana na malezi ya kizamani kuwanusuru watoto wao na dunia ya sasa yenye mambo mengi yanayohitaji usimamizi.
adiliko yaliyopo sasa uaminifu kwa baadhi ya wana ndoa umepungua kutokana na ongezeko la migogoro ya familia jambo ambalo limekuwa likisababisha watoto kulelewa na mzazi mmoja.
"Takwimu ambazo zimechukuliwa kwenye madawati ya jinsia kwenye maeneo mbalimbali baada ya watu kwenda kuripoti, zinaonyesha kwamba kila saa moja ndoa 13 zinaripoti migogoro, huku kasi ya talaka ikiongezeka."
Anaongeza: "Ndoa awali ilikuwa inaaminika kuwa msingi mzuri wa kulea watoto lakini kwasasa tunalalamika, na hao baadhi ya viongozi ambao tunawalalamikia kwasasa wametoka kwenye familia gani? Vijana vibaka wanatoka wapi, hao wote ni kwenye ndoa ambazo nyingi zimeingia migogoro na watoto wanalelewa humo au kuachwa wenyewe," anaeleza Annastazia.

UKURASA 11

# Nipashe

Jumanne Septemba 5, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581424
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US

UPATIKANAJI MAFUTA

# Vituo vyafungiwa, kashfa kuyaficha

## YALIYOMO

UKURASA WA 7
**SPIKA ATOA NENO WALIOTEMWA UWAZIRI**
SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson amewatoa hofu mawaziri walioondolewa katika Baraza...

UKURASA WA 17
**ACT -WAZALENDO YATAKA UBIA WAZAWA, DP WORLD**
CHAMA cha ACT -Wazalendo kimependekeza kampuni maalum ya wazawa itakayoingia...

UKURASA WA 20
KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA
**MJADALA MKALI KIZIMBANI UHALALI UMILIKI MAGARI YA BILIONEA MSUYA**
MAGARI manne ya kifahari yaliyodaiwa kuwa yamebadilishwa umiliki kutoka kwa...

## Wadau waainisha utajiri utakaobaki nchini Tanzania

UKURASA 19

UKURASA 17



Wananchi wa mjini Njombe wakiwa katika foleni kwenye moja ya vituo vya mafuta jana, lakini baadaye waliambiwa yamekwisha. **PICHA: ELIZABETH JOHN**

## Mwanasiasa mkubwa aingia matatani, kuburuzwa kortini

UK.2

**MICHEZO** SIMBA KUIGEUZA DYNAMOS DARAJA LA AL AHLY UK.24

**KATUNI** UK.6



Amiri Jeshi Mkuu Rais Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na viongozi wa Jeshi la Polisi baada ya kuwasili kwenye Bwalo la Maofisa wa Polisi (Police Officer's Mess) Oysterbay jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Rais ashtuka vitambi polisi

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemwagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camilius Wambura, kuhakikisha maofisa na maaskari wote wa jeshi hilo wanakuwa na mwonekano wa miili ya wastani na sio vitambi.

Lengo ni kuwawezesha kufanya majukumu yao ipasavyo muda wowote na mazingira yoyote, ikizingatiwa nchi inaelekea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu 2025.

Alisema jeshi hilo, mbali na kupewa mafunzo ya kitaaluma, pia lijikite katika kuwaimarisha kimwili kwa kuwapa mazoezi kila mara, ili wayakabili majukumu yao wakati wowote, ikiwamo wakati wa uchaguzi.

Rais Samia aliyasema hayo jana, wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Maofisa Wakuu Waandamizi wa Jeshi la Polisi nchini, uliofanyika Oysterbay, Dar es Salaam, huku akilitaka jeshi hilo kutosita kumchukulia hatua mtu au kikundi chochote ambacho kina lengo la kuvunja sheria za nchi.

"Serikali imetoa fedha kwenye jeshi na vitendea kazi, ili kuliwezesha lisimamie kazi zake vizuri hasa uchaguzi mwakani katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wasimamie haki, usalama na ulinzi na Uchaguzi Mkuu. Msisite kwa yeyote anayetaka kuvunja sheria za nchi, ili mradi anavunja sheria.

"IGP jenga jeshi lako kwenye miili, jenga zaidi kwenye miili, ukitazama hapa vitambi vinakuja kidogo, pamoja na mafunzo ya kitaalamu pia miili, inapokuja mchakamchaka uchaguzi unakuja kuna mbinu nyingi za kwenda kusafiri sana, ukianza kuhema hatutafika," alihadharisha.

Mbali na suala hilo, Rais Samia aligusia masuala mengine kadhaa yakiwamo malalamiko toka kwa wananchi kuhusu jeshi hilo, hasa ubambikaji kesi, akisema suluhisho linakuja ambalo ni Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Kuhusu madeni ya jeshi hilo kwa serikali, Rais Samia alisema: "Mwaka 2021 hadi 2022, mwaka 2023 tumejitahidi kuongeza bajeti na mwaka jana tumekwenda vizuri, ila tuna malimbikizo ya si chini ya Sh. bilioni 70. Kuna changamoto, haya ni madeni ya nyuma, kufanyia kazi madeni ya nyuma kiuhasibu kuna changamoto zake.

"Tunafahamu wapo ambao walikwishastaafu, wamelipwa mafao yao, lakini wana madai ya nyuma, hatutaki kumdhulumu mtu, tutalipa ila inahitaji kuhakikisha ni kweli madeni hayo," aliongeza.

Alilitaka jeshi liendelee kutumia TEHAMA na miradi tofauti itaendelea kufanyika, pia waimarishe ubunifu hasa kwa wanafunzi kwa kuwafundisha mbinu tofauti za kuwa na uzalendo.

Rais Samia pia alilitaka jeshi hilo kuimarisha dhana ya ulinzi shirikishi kwenye jamii, ili kuongeza usalama ingawa serikali itaendelea kuongeza bajeti, kuinua mazingira ya kazi, maslahi, matumizi ya TEHAMA, akihimiza pia waimarishe uadilifu.

"Samaki akianza kuharibika, mwangalie kwenye kichwa, ukimfunua hivi utajua huyu si mzuri, lakini akiwa mwekundu unajua samaki mzima. Sasa huku kwenye kichwa nako kumeanza kubadilika, mkibadilika makamishna, wasaidizi wale kule chini watabadilika.

"Wanaofanya mambo ya ajabu kule chini wakiona ninyi mnafanya vizuri, nao nwatabadilika. Unaweza kurushiwa 'clip' hadi unaona aibu, unaambiwa huyu ni wa Jeshi la Polisi, IGP kaza buti jeshi linyooke," aliagiza.

Mkuu wa Nchi pia alizungumzia vitendo vya rushwa, akisema bado kuna tatizo na kwamba mabadiliko ya TEHAMA yanakwenda kuliondoa hilo.

"Mfano, tukaweka kamera kwenye barabara zetu, ukaambiwa hakuna haja ya askari kusimama barabarani, aliyefanya makosa atajulikana, faini hii hapa kalipe," Rais alisema.

Awali, Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, alisema Sheria ya Serikali za Mitaa, inaelekeza kuimarishwa kwa shughuli za ulinzi na usalama, hivyo kila mkoa uhakikishe unatimiza hilo ili kuondoa uhalifu.

IGP Wambura alibainisha kuwa, katika kuboresha taasisi za ulinzi na usalama nchini, kuundwa kwa Tume ya Haki Jinai kumesaidia kupatikana mapendekezo ambayo yameanza kufanyiwa kazi, ili jeshi hilo kubadilika kwa utashi.

Kaulimbiu ya mwaka huu ya mkutano huo wa mwaka ni 'Matumizi ya TEHAMA Kuleta Uwazi, Mageuzi ya Jeshi la Polisi'.

## Kampuni yatishia kumshtaki mwanasiasa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Uwekezaji Sekta ya Utalii na Ranchi za Wanyama, Mwiba Holdings, imetishia kumchukulia hatua za kisheria mwanasiasa mmoja kwa madai ya kutoa tuhuma za uongo kuhusu tajiri wa Kimarekani kuwa na umiliki wa ekari milioni sita katika mbuga za Tanzania kwenye mikutano ya hadhara anayoendelea kuifanya Kanda ya Serengeti.

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na kampuni hiyo ambayo haikutaja jina mwanasiasa huyo, amekuwa akitoa madai hayo kupitia mikutano ya kisiasa mikoa tofauti ya Kanda ya Ziwa.

Kampuni ya Mwiba imetoa karipio kali kwa wote wanaotoa tuhuma dhidi yake na kuwataka waache mara moja kufanya hivyo au watalazimika kuchukua hatua za kisheria ili kulinda heshima na hadhi yao katika jamii.

"Baada ya ufafanuzi huu, tunawataka wale wanaozusha na kusambaza taarifa hizi za uzushi na uongo kuacha mara moja kufanya hivyo la sivyo tutalazimika kuchukua hatua kali za kisheria," ilisema sehemu ya taarifa hiyo iliyosainiwa na Mkurungenzi wa kampuni hiyo, Abdulkadir Luta Mohamed.

Taarifa ya Mwiba Holdings ilieleza tuhuma za uongo na uzushi dhidi yake zilitolewa kwenye mikutano ya hadhara iliyofanyika kwenye maeneo ya Sirari, Shinyanga na Kahama tarehe 11, 25 na 26 mwezi Agosti, mwaka huu.

Taarifa hiyo imedai kuwa tuhuma hizo zimetolewa mikoa tofauti kwenye mikutano ya hadhara kwa kipindi cha mwezi mmoja.

"Tajiri wa Kimarekani anaitwa Thomas Dan Friedkin anamiliki ekari milioni sita za ardhi katika maeneo ya hifadhi ya Tanzania.

Kuna taarifa kuwa wamegawa ekari milioni sita za mbuga ya wanyama kule Meatu kwa bilionea wa Kimarakeni anayeitwa Dan Friedkin."

Katika taarifa yake Kampuni ya Mwiba imekanusha kumiliki ardhi yoyote kwenye maeneo ya hifadhi nchini Tanzania na kwamba jumla ya eneo lote walilopangishwa wilayani Meatu ni ekari 171,604 na maeneo yote kisheria yanamilikiwa na halmashauri za vijiji ambako yapo.

Kwa mujibu wa takwimu za Mkoa wa Simiyu ambazo gazeti hili imeziona mitandaoni, mkoa mzima una eneo la kilomita za mraba 23,807 sawa na takribani ekari milioni 2.4. Eneo la Wilaya ya Meatu lililoko kwenye hifadhi ni kilomita za mraba takribani 4,253 sawa na ekari 425,000.

Takwimu hizo kwa madai ya mwanasiasa huyo zinamaanisha Mwiba imepewa eneo mara 14 ya eneo lote la hifadhi wilayani Meatu, na mara tatu ya ukubwa wa mkoa wote wa Simiyu.

"Jumla ya eneo lote lililopangishwa kwa kampuni ya Mwiba Holdings Limited wilayani Meatu ni kiasi cha ekari 171,604 na siyo ekari milioni sita kama inavyodaiwa na wazushi," ilisema taarifa hiyo.

"Mikataba miwili ya upangaji inahusu ranchi mbili za wanyamapori moja na Halmashauri ya Kijiji cha Makao na mwingine tumeingia na Halmashauri ya Kijiji cha Mwangudo. Ranchi zote hizo kisheria zinamilikiwa na vijiji vya Makao na Mwangudo," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kampuni ya Mwiba Holdings katika taarifa yake ilisema haijaingia mkataba wowote (moja kwa moja au kupitia kwa mtu au taasisi nyingine) na Serikali ya Awamu ya Sita.

Mikataba yote ya upangaji ya uwekezaji iliyotajwa hapo juu imekuwapo kwa muda mrefu na iliongezewa muda mwaka 2018 na 2019 wakati wa utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano.

Mwanasiasa huyo anadaiwa kusema tishio linalowakabili wananchi waishio karibu na maeneo ya hifadhi kuondolewa kwenye maeneo yao kwa kunyang'anywa ardhi zao kwa kile alichokiita kuwa ni maeneo ya hifadhi hizo kumilikishwa tajiri wa kimarekani, Dan Friedkin.

Alitaja taarifa hizo kuwapo katika mitandao ya kijamii na kuwa wananchi wanahoji umiliki wake wa ardhi nchini huku jamii za watu wanaoishi katika maeneo husika wakiendelea kunyanyasika na kufukuzwa katika maeneo yao halisi.

## MWIBA HOLDINGD LIMITED

# TAARIFA KWA UMMA

## TUHUMA ZA UONGO NA UZUSHI DHIDI YA KAMPUNI YA MWIBA HOLDINGS LIMITED NA THOMAS DAN FRIEDKIN

Wamiliki, akiwemo Thomas Dan Friedkin, na uongozi wa kampuni ya Mwiba Holdings Limited wanakanusha taarifa za uongo zilizotolewa kwenye mikutano ya hadhara ya kisiasa iliyofanyika Agosti 11, 25 na 26, 2023 huko Sirari, Shinyanga na Kahama zilizodai kuwa Serikali ya Awamu Sita imeipa Kampuni Holdings Limited umiliki wa ekari milioni 6 za eneo la hifadhi ya mbuga ya wanyama lililopo wilayani Meatu mkoani Simiyu.

Ukweli ni kuwa kampuni ya Mwiba Holdings Limited HAIMILIKI eneo lolote kwenye maeneo ya hifadhi nchini Tanzania. Katika Wilaya ya Meatu, Mwiba Holdings Limited ina mikataba miwili ya UPANGAJI (lease) na mkataba mmoja wa UWEKEZAJI (Investment) kama ifuatavyo:

a) Mikataba miwili ya UPANGAJI wa ranchi za wanyamapori: wa kwanza, Mwiba Holdings Limited imeingia na Halmashauri ya Kijiji cha Makao; na wa pili imeingia na Halmashauri ya Kijiji cha Mwangudo . Ranchi zote hizi kisheria zinamilikiwa na vijiji vya Makao na Mwangudo, mtawalia.

b) Mkataba mmoja wa uwekezaji kwenye kitalu cha uwindaji wa kitalii ambao Mwiba Holdings Limited imeingia na Jumuiya ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Makao. Kitalu hiki kinamilikiwa na vijiji saba: Makao, Ginano, Mwabagimu, Saapa, Mwangudo, Iramba-Ndogo na Mbushi.

Jumla ya eneo lote LILILOPANGISHWA kwa Kampuni ya Mwiba Holdings Limited Wilayani Meatu ni kiasi cha ekari 171,604 na si ekari milioni 6 kama inavyodaiwa na wazushi.

Kampuni ya Mwiba Holdings haijaingia Mkataba wowote (moja kwa moja au kupitia kwa mtu au taasisi nyingine) na Serikali ya Awamu ya Sita. Mikataba yote ya UPANGAJI na UWEKEZAJI iliyotajwa hapo juu imekuwepo kwa muda mrefu na iliongezewa muda 2018 na 2019 wakati wa utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano.

Baada ya ufafanuzi huu, tunawataka wale wote wanaozusha na kusambaza taarifa hizi za uzushi na uongo kuacha mara moja kufanya hivyo la sivyo tutalazimika kuchukua hatua kali za kisheria.

Abdulkadir Luta Mohamed
Mkurugenzi
September 4, 2023

**PO Box 2782 • Arusha • Tanzania**
**Phone: +255 27 297 0341 • Email: info@friedkintz.co.tz**

# MATANGAZO

217584402

217584402

Mtn 14/09/2023

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF SHINYANGA
*(AT SHINYANGA)*

CRIMINAL CASE NO. ..........16.......... OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

MASUNGA MLYELA MIZINGO ..................................... ACCUSED PERSON

To:

Masunga Mlyela Mizingo
Plot No. 2186, Block A
Majengo, Sokola – Kahama Road, Kahama DC
**Shinyanga Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT, CAP. 235 OF THE LAWS AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the ...14th... day of ...September...... 20 23 .....at **08:00 am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

Herein fail not.

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this ...17th...... day of ...August......... 202 23.

THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT, SHINYANGA — TANZANIA

.......................................
RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
P.O. BOX 29 - SHINYANGA

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**
Name ......................................

Signature ......................................

Qualification/Relationship
Date ......................................

217584402

217584402

# MATANGAZO



217584402



217584402



217584402



217584402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mkutano AGRF utumike kupata fursa sekta kilimo

**MKUTANO** wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF), unaanza leo nchini na unakutanisha zaidi ya watu 3000 kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika.

Kwa Tanzania ni mara ya kwanza kwa mkutano huu kufanyika na utatoa fursa kubwa kwa Watanzania kuutumia kama njia ya kupata masoko ya mazao yanayozalishwa nchini.

Mbali ya kilimo kuna fursa katika sekta ya mifugo, uvuvi na utalii sekta ambazo zinategemewa kwa kuingizia nchi mapato.

Mkusanyiko wa watalaamu wengi watakaohudhuria mkutano huo, utasaidia Watanzania kukuza kilimo chao kupitia mafunzo yatakayotolewa kutoka kwao na vilevile ni njia ya kutengeneza mtandao utakaowasaidia kuendelea kupata utalaamu wao hata watakapokuwa kwenye nchi zao.

Kupitia mkutano huo makundi maalumu hasa ya vijana na wanawake, yatapata fursa ya kujifunza kutoka mataifa mengine kuhusu teknolojia ya kufuga kisasa ili kupata mifugo bora itakayowawezesha kupata soko zuri.

Mkutano huo muhimu utasaidia sekta mbali mbali wakati washiriki watakapokuwa nchini, kwanza upande wa biashara, hoteli nyingi zitapata wageni ambao watasaidia kuingiza fedha za kigeni kutokana na malipo ya hoteli watakazopitia.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inatarajiwa kila mshiriki mmoja atatumia si chini ya Dola ya Kimarekani 500 (Sh. milioni 1.248) na watakaotembelea Jiji la Dar es Salaam, wataingiza si chini ya Dola 800.

Wapo wageni watakaokwenda kutembelea visiwa vya Zanzibar kujionea fursa za uwekezaji katika uchumi wa buluu ambao pia wanatarajiwa wakiwa huko wataingiza fedha za kigeni.

Wafanyabiashara na wajasiriamali watapata fursa ya kuuza bidhaa zao na kuzitangaza na vilevile kupata soko la nje.

Ni vizuri wafanyabiashara na wajasiriamali wakatumia fursa hiyo kujitangaza vizuri ili waendelee kuuza biashara zao kisasa kwa kutumia mitandao.

Tanzania imebarikiwa kuwa ardhi nzuri inayokubali mazao mengi, hivyo mkutano huo utawapa mwanga wa uzoefu wa nchi zingine zinavyoweza kuhifadhi vyakula vyao ili viweze kutumika kwa miaka mingi pale kunapokuwa na ziada ya kutosha na vilevile jinsi ya kuchakata ili kuviongezea thamani zaidi.

Kuna mazao yanayozalishwa nchini ambayo yana thamani kubwa yanapopelekwa nchi za nje kutokana na ubora wake, likiwamo zao la korosho ambalo linapendwa sana.


Kahawa ya Tanzania inasifika kwa ladha nzuri na hata wageni wanaokuja kutembea nchini wanaporudi kwao huinunua kwa wingi ili kwenda kuitumia nchini kwao.

Wazalishaji wa mazao hayo wanaweza kutumia fursa hiyo kuleta bidhaa zao na kuzitangaza zaidi ili kuendelea kufanya biashara kimtandao.

Dunia ya leo kila kitu kimebadilika, badala ya kutegemea njia moja ya kutafuta soko, sasa linatafutwa pia kimtandao na kuitangaza kwa njia hiyo inatoa fursa ya kuonekana na watu wengi duniani na soko linapanuka ziaidi.

Fursa hii ambayo Tanzania imepata ya kupata wageni wengi washiriki wa mkutano huo isiachwe ikapita bila nchi kunufaika. Kupitia mkutano huo watanzania watajifunza mambo mengi yatakayoleta manufaa kwa taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni njia ya kumkomboa kijana ikitiliwa mkazo



Na Sabato Kasika

**UBUNIFU** katika elimu ya ujasiriamali, una faida kwa vijana wanaohitimu elimu ya ngazi mbalimbali, iwapo watauzingatia, kwani wanaweza kubobea katika somo la ujasiriamali na kuwa wabunifu na wabobezi wakamudu maisha.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, elimu ya ujasiriamali inajikita katika kuvumbua vitu vipya, hivyo wahitimu wanaweza kusaidia kubuni na kuvumbua bidhaa na miradi mbalimbali yenye tija inayoweza kufungua ukurasa mpya wa maisha yao.

Miradi hiyo inaweza kuwa na faida kwao na kuwasaidia kujikimu kimaisha hata jamii na taifa kwa ujumla, kwani zipo rasilimali nyingi zinakosa watu wenye uwezo wa kufikiri matumizi yake.

Iwapo elimu ya ujasiriamali itatolewa, inaweza kuruhusu au kusaidia rasilimali mbalimbali zilizopo kutumika kwa ufanisi, na hivyo kuwafanya vijana wa Kitanzania kunufaika kwa elimu hiyo.

Ninaamini kwamba, kupitia elimu ya ujasiriamali tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana wa Kitanzania wanaohitimu ngazi mbalimbali ya elimu linaweza kupungua, kwani watakuwa na uwezo wa kubuni miradi mbalimbali ya maendeleo na kufanya wajikwamue kiuchumi.

Lakini pia, elimu ya ujasiriamali inaweza kuwa kichocheo kikubwa cha kukua kwa sayansi na teknolojia kupitia uvumbuzi na ugunduzi unaofanywa na vijana wajasiriamali. Elimu ya ujasiriamali ingefaa kuchukuliwa kama msingi kwa vijana kujiandaa kujiajiri, ili kupunguza wimbi la ukosefu wa ajira kwa vijana ambalo serikali imekuwa ikipambana nalo.

Bahati nzuri serikali imeliona hilo na sasa imeanza mkakati ya kuhakikisha somo la biashara linakuwa la lazima, kama njia ya kuwaanda vijana wa kubuni na kuendesha miradi yao waweze kufanya hivyo.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekusudia kufanya somo hilo kuwa la lazima kwa wanafunzi wote wa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne kwa mikondo yote miwili ya Elimu ya Jumla na Elimu ya Amali.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Elimu wa wizara hiyo Omari Juma Kipanga, wizara iko katika hatua za ukamilishaji wa mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 na Mitaala katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu.

Aidha, anasema wizara vyuo vikuu vimeelezwa kuhuisha na kufanya maboresho ya mitaala yote iendane na Dira na Mipango ya Maendeleo ya Taifa kwa kutoa elimu itakayompa kijana wa Kitanzania ujuzi.

Ni wiki iliyopita, bungeni jijini Dodoma, Naibu Waziri alitoa maelezo hayo wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Zainabu Katimba aliyetaka kujua lini serikali itaboresha mitaala ya elimu ili mafunzo ya biashara yatolewe kuanzia shule za msingi.

Anafafanua kuwa kuanzia darasa la kwanza hadi la saba, mitaala imetilia mkazo elimu ya fedha na ya ujasiriamali, na kwamba elimu hiyo imewekwa kwenye somo la hisabati, huku elimu ya ujasiriamali ikiwa kwenye somo la sanaa na michezo, lugha, jiografia na mazingira.

Anasema vyuo vikuu vya serikali na binafsi kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), vimepata mafunzo mbalimbali ya kuandaa programu zinazoendana na vipaumbele vya nchi na mahitaji ya soko la ajira.

Vilevile anafafanua kuwa kupitia utaratibu huo, zaidi ya programu 300 zitaanzishwa au kuhuishwa, ikiwamo somo la biashara ili kuendana na mahitaji ya sasa ya kijamii, kiuchumi na soko la ajira.

Kwa mkakati huo wa serikali ninadhani ukosefu wa ajira kwa vijana wanaohitimu elimu katika ngazi mbalimbali, unaweza usiwe kikwazo tena kwao kwa siku za usoni, iwapo watazingatia somo hilo.

# ATCL kupata ndege mpya mwezi huu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL) linatarajia kupata ndege mpya moja aina ya Boeing B737-9MAX mwishoni wa mwezi huu.

Vilevile, matengenezo ya ndege ndogo aina ya Dash 8 Q300 yanatarajiwa kukamilika na kurejea katika ratiba zake za utoaji huduma.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Gando (CCM), Mussa Omar Salim.

Mbunge huyo alihoji lini shirika hilo litaanza safari za Pemba, Kihenzile akijibu kuwa ATCL itaanza safari za Pemba baada ya kupata ndege za kutosha kutoa huduma bila kuharibu ratiba za safari za sasa na urukaji kwa wakati.

Alisema kuwapo ndege hizo kutaiwezesha ATCL kuanzisha safari zake katika kituo cha Pemba kwa tija na ufanisi.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji serikali lini itatoa kipaumbele kwa Pemba, Kihenzile akijibu kuwa serikali inatambua umuhimu wa kupeleka ndege hiyo ili wananchi wa Pemba watumie ndege hizo.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti maalum (CCM), Martha Gwau, alihoji lini kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Singida kitakamilika ili ndege zianze safari mkoani humo.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya, alisema mkoa huo uko karibu na Dodoma na serikali imeshafanya usanifu wa uwanja huo ili kutumika kama uwanja wa dharura endapo vya Dodoma vikipata changamoto.

# Spika atoa neno waliotemwa uwaziri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (pichani) amewatoa hofu mawaziri walioondolewa katika Baraza la Mawaziri hivi karibuni, akisema nafasi hizo ni za zamu na haina maana anayeondolewa ni mbaya.

Dk. Tulia pia amempongeza Naibu Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo ya kihistoria ambayo haijitokezi mara kwa mara na kuahidi kumpa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kiongozi huyo wa Bunge alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati wa kipindi cha 'Maswali', akisema chombo hicho kitaendelea kuwapa ushirikiano.

Alisema kuwa wapya waendelee kujifunza kwa waliotangulia. Waliopumzika kidogo wasiwe na wasiwasi kwa kuwa baraza lina watu ambao waliwahi kupumzika, wakarejea, wakapumzika tena, wakarejea.

"Kwahiyo, msiwe na wasiwasi. Hizi nafasi huwa ni kwa zamu, mtu zamu yake inapofika basi anapewa kufanya hiyo kazi. Zamu yake inapopungua kidogo, ni kama kocha anaweka huyu si kwamba wewe uliyetoka ni mbaya ama namna gani, bali kocha anataka kukupumzisha kwa ajili ya maandalizi ya shughuli nyingine hapo baadaye," alifafanua.

Aliongeza "...kama ni timu za Simba na Yanga, huenda timu inayokuja baadaye ikawa ni Namungo halafu ukapumzishwa kidogo ili wacheze na Namungo kwa sababu mechi inayokuja ni ngumu zaidi."

Kuhusu Dk. Biteko, Dk. Tulia alisema nafasi hiyo ni ya kihistoria kwa sababu haijitokezi mara kwa mara, hivyo Bunge litahakikisha linampatia ushirikiano wa kutosha ili wananchi waendelee kupata maendeleo.

"Tunakukaribisha sana bungeni ukiwa na nafasi nyingine sio kwamba wewe ni mgeni bungeni, lakini nafasi yako inatufanya tukukaribishe tena bungeni, karibu sana.

"Nitumie fursa hii kwa niaba yenu wabunge na wananchi wote kwa ujumla kukupongeza sana kwa imani ambayo Rais ameionyesha kwako kwa nafasi hiyo kubwa ambayo sote tunafahamu ni ya historia kwa sababu huwa haiji mara nyingi, inakuja mara chache.

"Waheshimiwa wabunge, Naibu Waziri Mkuu pia ni Waziri wa Nishati, hivyo kuna wakati atatakiwa kuja katika kamati, muwe mnakumbuka katika nafasi hizi sio mwanze kumwita kama ilivyokuwa kipindi cha nyuma, yatazameni yote hayo,"aliagiza.


Mtn i/c 07/09/2023

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA
(AT MWANZA)

CRIMINAL CASE NO. 23 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

GERALD YONA NZOWA ............ACCUSED PERSON

To:
Gerald Yona Nzowa
Plot No. 255, Block A,
Buhongwa Area,
**Mwanza City**

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT, CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 7th day of September 2023 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Herein fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 14th day of August 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name ............
Signature ............
Qualification/Relationship
Date ............

217584402



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF SHINYANGA
(AT SHINYANGA)

CRIMINAL CASE NO. 15 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

SIGI SHIGALU KALONGA ............ACCUSED PERSON

To:

Sigi Shigalu Kalonga
Didia Lohumbo Area
Shinyanga Rural District
**Shinyanga Region**

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT, CAP. 235 OF THE LAWS AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 14th day of September 2023 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Herein fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 17th day of August 2023

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
P. O. BOX 29 - SHINYANGA

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name ............
Signature ............
Qualification/Relationship
Date ............

217584402





Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, akisalimiana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Lucy Kabyemera, baada ya kuwasili kwa mara ya kwanza ofisi za wizara hiyo eneo la Mtumba jijini Dodoma. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Watoto 110 wazaliwa 'si riziki' robo mwaka

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WATOTO wachanga 117 mkoani Manyara, wamezaliwa wakiwa 'si riziki' na wengine kufariki dunia muda mfupi baada ya kuzaliwa katika miezi mitatu (robo mwaka) ya Aprili hadi Juni mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa Mkoa wa Manyara, Emma Ngatoluwa, watoto waliozaliwa 'si riziki' ni 74 na wengine 43 walifariki dunia muda mfupi baada ya kuzaliwa. "Chanzo cha vifo hivyo ni wajawazito kupata uchungu pingamizi, kuzalishwa na mtu ambaye siyo mtaalamu mzuri, kutembea umbali mrefu kufuata huduma na kutozingatia ushauri wa kitaalamu," alisema.

Mratibu huyo alitaka jamii kufuata ushauri wa wataalamu, hasa wajawazito kuhudhuria kliniki mapema na kwenda kujifungulia kituo cha afya au hospitali.

Akitoa ufafanuzi kuhusu hali hiyo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Catherine Magali, alisema wajawazito wengi wanaojifungua kwa mara ya kwanza au anayejifungua mimba ya tano na kuendelea, hupewa rufani ya kwenda hospitali kubwa ili wajifungue salama.

Hata hivyo, alisema kwa sasa kuna vituo vya afya vyenye uwezo wa kutoa huduma za kisasa kutokana na uwekezaji wa vifaa tiba.

Kwa mujibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) ya 2021/22-2025/26, uwekezaji wa serikali katika uhai wa mtoto umepunguza vifo vya watoto kati ya mwaka 2010 na mwaka 2015. Kiwango cha vifo vya watoto wachanga, kuanzia siku sifuri hadi siku 28 vimepungua kutoka vifo 40 hadi 25 kwa vizazi hai 1,000.

## Mauaji ya watu yashtua madiwani

**Na Dege Masoli,** KILINDI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga wamelitaka Jeshi la Polisi kutumia mbinu zake za medani kushughulikia matukio ya mauaji ya watu wilayani mwao, wanayodai yamekithiri.

Kwa nyakati tofauti jana, madiwani hao walishauri jeshi hilo kuongeza mbinu zitakazowezesha kubaini watu wanaotekeleza vitendo hivyo vya kikatili.

Akitoa msimamo wa baraza hilo baada ya madiwani kuchangia hali ya usalama wilayani mwake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, Idrisa Mgaza, alisema matukio ya mauaji ya mara kwa mara yamezusha hofu kubwa kwa jamii ya Kilindi.

Mgaza alieleza masikitiko yake kuhusu kukithiri matukio hayo ya mauaji, kuzusha hofu na kuchelewa kutiwa nguvuni watuhumiwa wa matukio hayo.

"Tunalitaka Jeshi la Polisi, sasa kuongeza mbinu za upelelezi na kuwabaini wahusika na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria ili kurejesha imani kwa wananchi.

"Matarajio ya baraza hili, ni kuona wahalifu wanakamatwa na matukio yanapungua kwa kasi," aliagiza.

Katika kikao hicho ambacho madiwani walitoa agizo hilo, Ofisa Tarafa ya Kwekivu, Michael John, alimwakilisha Mkuu wa Wilaya hiyo.

Akijibu baadhi ya hoja za madiwani, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Gordian Gwiyago, aliwahakikishia wajumbe wa baraza hilo kwamba uongozi wa halmashauri hiyo umejipanga kutekeleza maagizo yote yanayotolewa na madiwani kwa lengo la kufikia mafanikio.

# Tatizo la uvuvi haramu latafutiwa dawa

**Na Hamida Kamchalla,** MKINGA

WADAU wa Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu (MTRU) wameanza kutafuta 'mwarobaini' wa tatizo la uvuvi haramu na uchafuzi wa mazingira katika Pwani ya Bahari ya Hindi, hususani eneo la mwambao wa Moa lililoko Wilaya ya Mkinga, mkoani Tanga.

Ili kukabiliana na tatizo hilo, MTRU kwa kushirikiana na Shirika la Jamii ya Uhifadhi wa Wanyamapori (WCS), wameanza na kibarua cha kujenga uwezo kwa wadau wa eneo hilo, kuwapa jengo la ofisi, gari na vifaa vya kufanyia kazi ya kupambana na vitendo vya kiharamia vinavyoendelea baharini.

Jana, Mkurugenzi Mkuu wa WCS, Simon Lugandu, akizungumzia mkakati huo, alisema lengo la shirika hilo ni kufanya uhifadhi wa mazingira hasa wa bayoanuai.

"Lakini pia, tunalenga kuwakwamua kiuchumi wadau hawa na hivi sasa tayari tumekwishafanya miradi mingi katika mikoa tofauti. Tangu kuanza kwa shirika hili, tumeshatekeleza miradi ipatayo 150".

"Mingi kati yake ilihusu utafiti na mingine ni ya uhifadhi na katika misitu, kazi yake ni kuhifadhi mali asili ya wanyamapori na kwa upande wa bahari kuna hifadhi maliasili ya matumbawe na viumbe vilivyomo.

"Watanzania tuna bahati, takribani asilimia 40 ya maeneo tuliyonayo nchini yamehifadhiwa kwa njia moja au nyinginel Kwahiyo, tumefanya kazi kubwa katika kuhifadhi rasilimali tulizonazo na ni wajibu wetu".

"Ninasema hivi ili kuwaelezea msisitizo kama shirika la WCS, kwamba ni muhimu tukahifadhi rasilimali hizi kwa ajili yetu na vizazi vinavyokuja," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, Kanali Maulidi Surumbu, alisema wilaya hiyo kulikuwa na tatizo kubwa la uvuvi haramu, lakini serikali ilipofanya misako ya mara kwa mara, tatizo limepungua kidogo, ingawa bado wapo watu hawataki kuelewa.

"Sasa hivi tuna kila sababu ya kujipongeza kwa kuwa majanga yamepungua sana, lakini bado ayajaisha. Kwahiyo, kuwapo kwa vifaa hivi sasa kunakwenda kuongeza kasi ya kumaliza kabisa tatizo hili. Salamu ziwafikie wale wasiotaka kubadilika," alionya Kanali Surumbu.

Aliongeza: "Nitoe wito kwa wananchi wote wa Wilaya ya Mkinga ambao wanaendeleza vitendo vya uchafuzi wa bahari, wabadilike na waache kabisa, kwa kuwa vifaa vya kisasa vimekuja kuongeza nguvu na sasa hakuna kwa kujificha. Kwahiyo, niwaombe sana wananchi kuvitunza hivi vifaa kwa maslahi mapana ya nchi yetu," alisisitiza.


Kanali Surumbu alisema hifadhi ya mazingira ya bahari ni muhimu sana katika utunzaji wa rasilimali ya uvuvi, hususani katika mazingira yote yanapaswa kuzingatia kaulimbiu ya uvuvi, ambayo inazingatia mazingira.

"Na kwa kutambua hili, serikali iliamua kuanzisha hifadhi ya bahari na maeneo tengefu kupitia Sheria Na. 29 ya Mwaka 1994. Kwa sasa, maeneo ya bahari yaliyohifadhiwa nchini yamefikia ukubwa wa kilomita za mraba 2,220 sawa na asilimia 6.5 ya bahari ya ndani," alifafanua Kanali Surumbu.

Mratibu wa Mradi wa Uhifadhi wa Bahari, Jean Mensa, alisema kuwapo uhifadhi wa bahari na maeneo tengefu ni muhimu.

## TANGAZO


A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO
DRINKING WATER
FURAHIA MAISHA
NA MAJI ASILIA
500ml
1000ml
1500ml
6L
12L
18.9L
+255 659 536 937, +255 758 979 641, +255 659 785 276
kdw@bbl.co.tz
kilimanjarodrinkingwater
kilimanjaro_drinking_water
217584002





# Maonesho ya Madini kuifungua Geita kiuchumi

**Na Said Sindo,** GEITA

MAONESHO ya Sita ya Madini yanayotarajiwa kufanyika mkoani Geita, yanatajwa kuwa chachu na kufungua mkoa huo kiuchumi kwa kuongeza fursa mbalimbali za uwekezaji katika sekta ya hiyo na nyinginezo.

Inaelezwa kuwa maonesho hayo yatatoa fursa katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uzalishaji, utafiti na kwa waongezaji thamani ya madini ambao watakutana katika maonesho hayo watakaofika kujifunza na kuangalia fursa za uwekezaji.

Ofisa Uwekezaji kutoka Idara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Ofisi ya Mkoa wa Geita, Charles Chacha, alibainisha hayo alipozungumza na Nipashe ofisini kwake jana na kueleza kuwa wawekezaji kutoka ndani nan je ya Tanzania wanatarajia kushiriki katika maonesho hayo.

"Wataalam wengi na viongozi wakubwa waje kuona namna gani uchimbaji wa madini unaweza kufanyika bila kuathiri sana mazingira, na hata maeneo ambayo yameshathirika ni namna gani yanaweza kurekebishwa," alisema.

Chacha alisema kuwa katika maonesho hayo wanahitaji wachimbaji wadogo na wakubwa wajifunze teknolojia na kufanya utafiti kwa lengo la kudhibiti uchimbaji holela na kuhimiza uchimbaji katika maeneo yaliyofanyiwa utafiti na yenye uhakika wa madini.

"Tumetenga maeneo maalum, watu wanaolelewa na SIDO watakuwa na eneo lao, watu wanaolelewa na Chemba ya Wanawake (TWCC) watakuwa na maeneo yao. Machinga na wafanyabishara wa kawaida nao watakuwa na maeneo yao," alisema Chacha.

Maonesho ya Teknolojia ya Madini mkoani Geita yalianzishwa mwaka 2018. Katika maonesho ya mwaka jana, kulikuwa na washiriki 302. Mwaka huu maonesho hayo yanatarajiwa kuwa na washiriki zaidi ya 600 wa ndani na nje ya Tanzania.

Maonesho hayo mwaka huu yamebeba kaulimbiu isemayo 'Matumizi ya Teknolojia Sahihi Katika Kuinua Wachimbaji Wadogo Kiuchumi na Kuhifadhi Mazingira'.



Wakazi wa Kijiji cha Busekera katika Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara wakiwa kwenye mkutano wa hadhara uliohutubiwa na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Tundu Lissu jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Wenye ulemavu wasipimwe sawa na wengine kwa ufaulu'

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) mkoani Kagera, limeomba serikali kuweka utaratibu kutounganisha wanafunzi wenye ulemavu na wasio na ulemavu katika ufaulu.

Limesema kundi hilo linapaswa kupewa mchanganuo wake wa matokeo kutokana na changamoto walizonazo katika usomaji wao.

Hoja hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu wa shirikisho, Sweetbert Mshanga, alipozungumza na Nipashe kuhusu mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu.

Alisema ni kweli serikali imeweka ujumuishi katika masomo yao, lakini itambue kwamba wanafunzi hao wana ulemavu wa aina tofauti, ndivyo ilivyo hata katika uelewa wa masomo darasani. Hawezi kulingana na wengine.

Hata hivyo, Katiba ya nchi inazuia mtu kufanyiwa kitu chochote chenye ishara ya kumbagua kutokana na hali yake kimwili.

Katibu huyo alisema itapendeza ikiwa serikali inapotoa matokeo ya jumla, ichanganue na kuonesha idadi ya wenye ukamilifu wa viungo lakini, miongoni mwa matokeo hayo wenye ulemavu watajwe ni kadhaa.

Alisema hatua hiyo itamwonyesha mzazi kuwa kupitia ujumuishi walionao, yapo mafaniko katika elimu wanayoipata na kuwajengea imani kuwa mwanafunzi hayuko katika kuhesabu madarasa tu.

"Kama ufaulu ni mdogo, ijulikane nini mzazi atafanya kumkazia mwanawe pindi anapokuwa nyumbani. Vilevile, itasaidia kuwapa motisha wazazi na walezi wa watoto hao, hivyo kuwaendeleza zaidi kimasomo," alisema Mshanga.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Rugambwa iliyoko Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera, Witness Amos, wanatoa elimu kwa wanafunzi wote shuleni huko bila kujali aina ya ulemavu alionao mwanafunzi ili kuweka usawa katika masomo yao. Wote wanakuwa katika safari moja ya elimu.

Mwalimu Amos alisema muda wa masomo wanatakiwa kujifunza pamoja, japokuwa watu wenye ulemavu katika maendeleo ya taaluma yao wanakuwa hawafanyi vizuri sawa na wengine.

Alisema hali hiyo inatokana na tatizo la maumbile waliyonayo, lakini hawakatishwi tamaa. Lazima wapate muda wa ziada kujifunza tena.

"Nina imani kuwa wakifanya utafiti, wataweza kuwatolea mtihani unaoendana kwa tatizo la kusikia, kuona na kuongea sawa na mtu mwingine kwa kuwa uelewa wake unakuja taratibu na lazima apitishwe tena kwa umakini," alisema Mwalimu Amos.

Ofisa Elimu Watu Wazima katika mfumo rasmi mkoani Kagera, Fortunatus Kawa, alisema Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2004 inaelekeza kila mwanafunzi anatakiwa apelekwe shuleni na apatiwe elimu na kupewa mahitaji ya msingi kulingana na uhitaji alionao.

Alisema shule jumuishi ziliwekwa ili kuondoa ile hali ya kuonyesha utengano kati ya wanafunzi ambao hawana ulemavu na kuweka ushirikiano na wenye ulemavu kwa kuwa wote wanafanana katika masomo yanatolewa shuleni.

# Bilioni 10.6/- kukarabati barabara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) mkoani Shinyanga umetenga Sh. bilioni 10.6 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24 kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara.

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa TANROADS Mkoa wa Shinyanga, Mibara Nbilimbi, baada ya kupita na kukagua mizani iliyoko Mwendakulima, wilayani Kahama.

Alisema miongoni mwa mambo yanayochangia uharibifu wa barabara ni ubebaji mizigo iliyopitiliza kiwango, hali ambayo imekuwa ikisababisha serikali kutenga bajeti ya ukarabati wa barabara hizo kila mwaka wa fedha huku mwaka huu zikitengwa Sh. bilioni 10.6. "Tunatoa wito kwa madereva wa kubeba mizigo, wasizidishe uzito na kusababisha uharibifu wa barabara na kuingiza hasara serikali kutenga bajeti kila mwaka kufanya matengenezo ya barabara, Fedha hizi zingeelekezwa katika ujenzi wa barabara zingine," alisema Nbilimbi. Alitoa wito kwa wananchi kuendelelea kuitunza miundombinu ya barabara na kuacha kufanya shughuli za binadamu kando ya barabara zikiwamo shughuli za kilimo na kutong'oa alama za usalama barabarani.

Msimamizi wa Mizani ya Mwendakulima, Lugembe Vicent, alisema tabia ya madereva kuzidisha uzito wa mizigo imepungua tofauti na zamani. Kwa siku wamekuwa wanapima wastani wa magari 400.

Baadhi ya madereva wa magari ya mizigo, akiwamo Ramadhani Athumani, walisema tatizo la uzidishaji wa mizigo linasababishwa na matajiri wenyewe, pia madereva ambao siyo waaminifu - hubeba mizigo mingine njiani kwa tamaa ya kupata fedha.



Ukurasa 12

Jengo jipya Umoja Posta Afrika linavyoakisi mabadiliko kidijitali



Ukurasa 13

Midahalo waathirika ukatili ilivyo mwalimu bora kukabili wanyanyasaji

Nipashe
TESA
Jumanne Septemba 5, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

Ndivyo wachafuzi wakubwa mazingira kama hawa wanavyoendelea kuitesa Afrika

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mtaalamu atoboa siri kubomoka familia, utandawazi kunavyoumiza malezi, makuzi

• Kila saa moja ndoa 13 huingia migogoro, balaa kasi ya talaka

KUNA usemi kuwa samaki akunjwe angali mbichi, ukimaanisha kwamba mtoto anatakiwa kufundishwa vitu vingi kuanzia mwenendo mwema, maadili na elimu ya dunia akiwa mdogo si baada ya hapo.

Mtoto akifundishwa jambo akiwa mdogo ni rahisi kulishika na kulifanyia kazi lakini pia atakuwa na kumbukumbu kila anapoona anakwenda tofauti na maelekezo ya kile alichofundishwa na mlezi au mzazi na hata mwalimu.

Annastazia Rugaba ni Meneja Utetezi kutoka shirika la TWAWEZA, anayewakumbusha wazazi na walezi kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia na kuachana na malezi ya kizamani kuwanusuru watoto wao na dunia ya sasa yenye mambo mengi yanayohitaji usimamizi.

Akitoa mada katika Jukwaa la Ufahamu wa Kiraia linaloandaliwa na Shirika la Vijana la Youth Partnership Countrywide (YPC) wilayani Kibaha mkoa wa Pwani, anasema malezi ya karne ya 21 yanatakiwa kuwa na mabadiliko zaidi.

Anasema wazazi na walezi wanatakiwa kuwalea watoto kulingana na namna teknolojia ilivyobadilika ili kuwalinda na athari za mabadiliko ya kimaadili ambayo yanatishia karibu kila eneo la makuzi na malezi.

Makuzi ambayo yanahusisha mabadiliko ya kiakili, kimwili, kifikra na kijamii mtoto anayopitia katika hatua za ukuaji wake, huku malezi yakiambatana na uangalizi wa karibu wa wazazi au walezi kwa mtoto kiroho, kiafya, kiakili na kitabia.




Annastazia Rugaba akitoa elimu kwenye Jukwaa la Ufahamu wa Kiraia. **PICHA: JULETH MKIRER**

Annastazia anasema, teknolojia inavyozidi kukua inatakiwa kuendana na malezi ya watoto katika karne ya 21 ili kuwaepusha kujiingiza kwenye mambo ambayo hayaendani na maadili ya Mtanzania na jukumu kubwa liwe ni kufuatilia na kuwaepusha na kupotoka.

Anazungumzia mitandao ya kijamii imekuwa sababu ya mabadiliko kwa watoto wengi na hata kuiga mambo ambayo ni kinyume na maadili na kutishia hatma ya maisha yao.

Anasema kutokana na hali hiyo watoto wanatakiwa kulelewa na kufundishwa njia sahihi wakiwa bado wadogo wakue katika njia zilizonyooka na kuwa waelewe mema na mabaya na namna kama wakijiingiza kwenye ubaya unavyoweza kuathiri maisha yao.

Vile vile wazazi wanatakiwa kuwa waangalifu kwa vijana wao kwa kuwafuatilia kwenye matumizi ya simu, runinga pamoja na baadhi ya vinywaji ambavyo wakati mwingine vinaongezewa vitu vinavyowabadilisha mfumo kwenye miili yao.

Aidha, anasema "Malezi ya karne ya 21 ni shida isiyoelezeka kwenye mabadiliko ya kiteknolojia yanaenda kasi isivyo kawaida wazazi na walezi wanatakiwa waachane na kuwalea watoto kizamani mfano kuwapiga na kufoka muda wote, kuwadanganya huku wakiwaficha mambo muhimu kwa mfano suala ya mabadiliko ya miili yao na kujamiana katika umri mdogo.

Aidha, mimba, magonjwa ya kingono, ulawiti na ushoga, kuingiliwa kinyume cha maumbile wakidhani hawafahamu . Wabadilike ili kuwaepusha na kwenda kinyume na hali halisi" .

Anasema kutokana na mabadiliko yaliyopo sasa uaminifu kwa baadhi ya wana ndoa umepungua kutokana na ongezeko la migogoro ya familia jambo ambalo limekuwa likisababisha watoto kulelewa na mzazi mmoja.

"Takwimu ambazo zimechukuliwa kwenye madawati ya jinsia kwenye maeneo mbalimbali baada ya watu kwenda kuripoti, zinaonyesha kwamba kila saa moja ndoa 13 zinaripoti migogoro, huku kasi ya talaka ikiongezeka."

Anaongeza: "Ndoa awali ilikuwa inaaminika kuwa msingi mzuri wa kulea watoto lakini kwasasa tunalalamika, na hao baadhi ya viongozi ambao tunawalalamikia kwasasa wametoka kwenye familia gani? Vijana vibaka wanatoka wapi, hao wote ni kwenye ndoa ambazo nyingi zimeingia migogoro na watoto wanalelewa humo au kuachwa wenyewe," anaeleza Annastazia.

Anabainisha kwamba zamani kulikuwa na changamoto kwenye malezi lakini hazikuwa nyingi kama ilivyo sasa, mabadiliko hayo pia sambamba na migogoro ni sababu inayochangia siku hizi mabinti wengi kupata watoto bila ndoa kwa kuona taasisi hiyo haina haja tena .

"Mahusiano ya jinsia moja pia yameongezeka tunakokwenda hali inazidi kuwa mbaya. Dawa za P2 wanatumia mabinti kuzuia mimba kitu ambacho wataalamu wa afya wanasema usitumie zaidi ya mara mbili kwa mwaka na sasa wanaziona kama pipi jambo ambalo baadaye inakuwa na athari kubwa kwa watoto bila wao kujua," anaonya.

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA MWANDISHI MAALUM

# Jengo jipya Umoja Posta Afrika linavyoakisi mabadiliko kidijitali



Jengo jipya Umoja Posta Afrika (PAPU). **PICHA: TCRA**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, Septemba 2023 anaacha alama muhimu kwenye maendeleo ya sekta ya posta barani Afrika, pale anapofungua jengo la makao makuu ya Shirikisho la Umoja wa Posta Afrika -PAPU Tower, jijini Arusha.

Ujenzi wa PAPU Tower ni mfano wa mchango mkubwa wa sekta ya Posta Afrika kuelekea mabadiliko kidijitali ili kutoa huduma zinazoakisi ubora kwa wananchi.

Kupitia jengo la kisasa litakalokuwa makao makuu ya taasisi mahsusi kwa kushughulikia masuala ya posta ndani ya bara hili, ni udhihirisho kuwa hakuna kurudi nyuma.

PAPU inatekeleza mikakati ya kuendeleza biashara mtandao barani humu, na sasa imepata jengo la makao makuu lililojengwa kwa mabilioni na ambalo ni kivutio kwa usanifu na mwonekano wake, ulio kama stempu.

Kwa Arusha, jiji linalojulikana kwa sifa ya kuwa kituo cha mikutano ya kimataifa, ni johari nyingine kwenye taji lake, ikumbukwe Tanzania iijitolea kuwa mwenyeji wa PAPU umoja huo ulipoanzishwa Januari 1980 mjini Arusha.

Jengo hili jipya limejengwa kwa ubia kati ya umoja huo na Serikali ya Tanzania kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na kwamba umiliki ni asilimia 60 PAPU na asilimia 40 TCRA.

TCRA, msimamizi wa sekta ndogo ya posta nchini, ni mdau mkuu katika mradi huu na inawakilisha serikali kwenye masuala ya kuhudumia PAPU.

> Posta zinatakiwa kuchukua fursa ya kukua kwa biashara mtandao na masoko yanayojitokeza kuongeza vyanzo vya mapato yao na kujijengea uhalali miongoni mwa jamii zinapotoa huduma.

Kukamilika kwa jengo hili kumewezekana miaka mitatu baada ya kuwekwa jiwe lake la msingi, sherehe iliyofanyika Januari 2020, wakati wa maadhimisho ya miaka 40 ya PAPU. Aliyekuwa Waziri wa wa Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, ndiye aliweka jiwe hilo.

Jengo hili limebadilisha mandhari ya jiji la Arusha, mfano wa stempu ya kidijitali unaonekana kwa wanaoingia jiji hili kutoka sehemu tofauti na ukiwa juu yake unapumua hewa safi na kuona jiji kwa chini, ikiwa ni pamoja na ardhi na mashamba, miti na bustani na vijito vinavyotiririka maji kutoka Mlima Meru, ambao ni wa pili kwa urefu baada ya Kilimanjaro ulio jirani.

Majengo ya umoja huo yamejengwa katika mita za mraba 22,421, kando ya barabara kuu kutoka Moshi kuelekea Namanga kwenye mpaka wa Tanzania na Kenya. Arusha ni lango kuu cha kuingilia maeneo ya vivutio vya kitalii, vikiwa ni pamoja na mbuga ya wanyamapori ya Serengeti na eneo la uhifadhi la Ngorogoro, ambalo litambuliwa kimataifa kama Urithi wa Dunia.

Huduma nyingi kwenye jengo hilo zinaendeshwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa, ambazo zinawezesha mtumiaji kupata huduma kwa ufanisi wa hali ya juu.

Jengo kuu lenye ghorofa 17 lina sehemu ya chini ya ardhi, ofisi za kisasa, eneo la shughuli za biashara na maegesho yenye uwezo wa kuhifadhi magari 137, na kwamba chini ya ardhi yanaweza kukaa 37 wakati 130 ni maegesho ya kuzunguka jengo.

Aidha, kuna seti tatu za majenereta ya umeme kwa ajili ya dharura, matengi ya kufadhia maji -ya juu ya paa yenye uwezo wa ujazo wa lita 7,200 na chini ya ardhi yanayobeba lita 210,000.

Vilevile kuna ukumbi wa mikutano wenye vifaa vya kisasa vya kidijitali, unaoweza kuingia washiriki 400 kwa mara moja. Pia kuna vyumba vitano vya mikutano midogo vyenye uwezo wa washiriki 30 kila kimoja.

Uamuzi wa kuwa na jengo la kisasa la PAPU ulifanyika kwenye mkutano wa 29 wa kawaida wa mawaziri wa uliokuwa Umoja wa Nchi Huru Afrika (OAU), ambao sasa ni Umoja wa Afrika (AU) Julai 1977 jijini Libreville,Gabon. Walipitisha azimio namba CM/ Res. 586(XXIX) ambalo lilipendekeza kuanzishwa kwa PAPU kuwa chombo cha juu cha kusimamia masuala ya Posta Afrika.

Oktoba 1984, PAPU na Serikali ya Muungano wa Tanzania ziliingia mkataba ulioainisha masharti na vipengele vingine vya kuweka makao makuu ya umoja huo Arusha. Hili lilifuatia kutolewa idhini na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere Septemba 1984, hivyo kufungua njia ya kuwa na makao yake makuu Arusha.

Kwa kipindi kirefu, huduma za Posta Afrika zimekuwa na majukumu ya kipekee, kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya uhuru.

Katika ujumbe wake siku ya Posta Afrika Januari 18, 2023, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alieleza kwamba ushirikiano baina ya nchi kupitia huduma za posta umekuwa na umuhimu mkubwa katika kujenga mazingira ya biashara. Ili kufanikisha na kuwezesha hili, Tanzania hivi karibuni imekaribisha uwezeshaji wa huduma za posta kati yake na nchi nyingine kupitia mipaka.

PAPU inasisitiza utayari wake wa kubadili huduma za Posta Afrika kuwa kichocheo cha biashara mtandao kati na baina ya nchi.

Katibu Mkuu wa umoja huo, Sifundo Chief Moyo, anasema kwenye ujumbe wa siku hiyo, kwamba hili litawezekana kupitia mabadiliko ya kidijitali katika uendeshaji shughuli za posta na kuzifanya kuwa za kisasa kwa kutumia teknolojia ili kufungamanisha utoaji wa huduma.

"Posta imechukua mwelekeo tofauti kufuatia kushuka kwa idadi ya barua na kuongezeka kwa vifurushi vinavyosafirishwa kama sehemu ya biashara mtandao. Sekta ya posta inabidi kuelekeza juhudi zake, kupanga upya uwezo na mwelekeo wake na pia rasilimali zake, ili kujiweka tayari kutoa huduma kama chombo kinachotegemewa kusafirisha vitu na kufikisha huduma", anafafanua.

"Posta zinatakiwa kuchukua fursa ya kukua kwa biashara mtandao na masoko yanayojitokeza kuongeza vyanzo vya mapato yao na kujijengea uhalali miongoni mwa jamii zinapotoa huduma. Vituo vya posta zaidi ya 37,000 vilivyoenea Afrika ni sehemu za kuanzia kupanua huduma kupitia mifumo ya kidijitali kuelekea kuwa na posta zenye hadi za kisasa", anasema Katibu Mkuu Moyo.

"Kwa kupata na kutumia programu za kidijitali kuendesha posta na kutoa huduma kupitia intaneti na vifaa vya mkononi kama vile simu janja, vishkwambi, kompyuta mpakato, posta zinaweza kuongeza uwezo wa kutoa huduma kwa ufanisi zaidi." anaongeza.

ELIMU
NA SHABAN
NJIA, KAHAMA

# Midahalo waathirika ukatili ilivyo mwalimu bora kukabili wanyanyasaji

WATETEZI wa usawa wa kijinsia mikoa ya Shinyanga na Singida, wanaamini kutumia midahalo inayowakutanisha wananchi na kituo jumuishi cha waathirika wa ukatili (SHUFAA), ni njia mojawapo ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto wa mikoa hiyo.

Ikihusisha wananchi wanaoishi pembezoni na vijijini, mijadala hiyo inawapa taarifa, mikasa, mwanga, uzoefu na uwezo wa kutambua haki zao, madhara na namna ya kuripoti kwenye vyombo vya sheria hivyo kufungua ukurasa mpya wa kupambana na ukatili wa kijinsia.

Midahalo hiyo inayosimamiwa na mashirika ya kiraia yanayofanyakazi na serikali katika kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia yanayowanyima haki wanawake na watoto hususani kukosa elimu na kulazimishwa kuingia kwenye ndoa wakiwa na umri mdogo.

Kamishna wa Polisi Jamii, Faustine Shilogile, wakati wa akizindua kituo cha kuhudumia waathirika wa ukatili Kata ya Bugarama Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga hivi karibuni, anasema, matukio ya ukatili kitaifa yanaongezeka na kwamba yalifikia 30,566 kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na 1,193 yaliyoripotiwa mwaka 2021.

Aidha, anasema mwaka 2022 matukio ya ukatili wa kijinsia kwa watoto wadogo yalikuwa 12,163 ikilinganishwa na 11,419 kwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la matukio 670 hivyo juhudi za kukabiliana na wimbi hilo hazikwepeki , ikiwamo kufanya midahalo ya mara kwa mara.

Wadau wanaokabiliana na tatizo hilo ni Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), wakisimamia mhadalo shirikishi ndani ya jamii kupitia mradi wa kushirikisha jamii kwa lengo la kutokomeza ukatili na mila desturi kandamizi.

Kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa ya (KOICA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) na la Wanawake (UN-WOMEN), wamekuja na mbinu hiyo inayolenga kuibua na kuripoti wahusika.

Ofisa kutoka (TGNP) Jackson Malangila , anasema, wamekuja na mbinu mpya ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia katika familia na jamii kwa kuanzisha mihadalo mbalimbali itakayowapatia fursa wananchi kutoa maoni kwa uwazi na uhuru kwa kile wanachofanyiwa badala ya kukaa nacho moyoni.

Anasema, mihadalo hiyo inashirikisha wananchi wa kata zote 18 za Halmashauri ya Msalala, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, watendaji wa vijiji na kata, wenyeviti wa vitongoji na vijiji pamoja na wasaidizi wa kisheria ambao wanatoa elimu ya ukatili na madhara yake na namna wanavyotoa msaada wa kisheria kwa wahanga.

Aidha, Malangila anasema, walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari wanawajibu wa kuanzisha klabu ili kuleta matokeo chanya kwasababu moja ya sifa ya mradi ni kujumuisha makundi mbalimbali katika jamii ili kuwa sehemu ya kupata sauti kwa wenzao wenye jinsi ya kike.

"TGNP inasimamia midahalo hii ili kuwajengea uwezo wanafunzi kujua namna bora ya kupinga vitendo vya ukatili ambavyo husababisha madhara makubwa na kuwakosesha masomo yao, kama suala hili halitapatiwa suluhisho ukatili bado utaendelea kufanyika na kuwaumiza wanawake na watoto"anasema Malangila.

### WANAFUNZI WAAMKA

Godfrey Tinya, mwanafunzi wa kidato cha tatu Shule ya Sekondari Lunguya anasema, kuna baadhi yao wanapofika darasa la saba na kidato cha nne hushawishiwa na wazazi na walezi wafanye mitihani vibaya ili wakaozeshwe au kuozwa hali inayosababisha kukosa haki zao za kielimu.

Anasema, kuna wanafunzi wawili waliacha masomo yao wakiwa kidato cha tatu na kukimbilia maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu na kuchota maji ya kusafisha madini hayo, lakini kwa elimu ya ukatili wa kijinsia waliyiopewa na (TGNP) wamewarejesha na sasa wanaendelea na masomo.

Godfrey anawataja wanafunzi hao kuwa ni pamoja na Jackson Amosi(19) pamoja na Kulumuna Nicholaus(18) walioacha masomo kwa miezi sita wakiwa kidato cha tatu na sasa wapo kidato cha nne wakijiandaa na mitihani ya mwisho na wamekuwa mabalozi wazuri wa kupinga utoro.

"Tuliunda klabu shuleni na kufanya midahalo ya mara kwa mara ya ukatili na moja ya maazimio yetu ilikuwa kuwarejesha wanafunzi wote waliokimbia masomo iwe kwa kuolewa au waliolekea migodini, tumewarejesha wanafunzi wawili na sasa wako kidato cha nne." Anasema.



Kaimu Mkurugenzi wa KOICA Heo Eun, akizungumza na wanakata ya Bugarama mkoani Shinyanga, wakati wa ufunguzi wa kituo jumuishi cha waathirika wa ukatili **PICHA: SHABAN NJIA**

Kulumuna ambaye aliacha shule na kwenda machimboni anasema, baada ya wanafunzi wenzie kumfuata na kumweleza faida za elimu alikubali kurejea darasa ili kutimiza ndoto zake za kulitumikia taifa , akitamani kuwa mhandisi sekta ya madini akidai alikimbia masomo kwa ugumu wa maisha na wazazi wake kutokuwa na mwamko wa elimu.

### MAMIA WAFIKIWA

Heo Eun, ni Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la Watu wa Korea (KOICA), anayesema wanawake na watoto 10,000 wamefikiwa na kupatiwa elimu ya ukatili wa kijinsia, madhara yake na kuhakikisha wanatoa taarifa ya vitendo hivyo vinavyofanyika ndani ya familia kwa lengo la kukabiliana nayo yasiendelee kujitokeza.

Anasema,watu hao ni kutoka katika Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga na Ikungi mkoa wa Singida, hivyo kila aliyefikiwa atakuwa akitoa taarifa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi ili kukomesha vitendo hivyo. Anawataka kinamama kuachana na tabia ya kuogopa kutengwa na familia pale atakapobainika kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia.

Naibu Mwakilishi Mkazi wa UNFPA, Melissa Barret, anasema uwepo wa vituo hivi kumesaidia jamii kuwa na ufahamu kuhusiana na madhara ya ukatili, unyanyasaji wa kijinsia pamoja na namna bora ya kuripoti taarifa na kumlinda mhanga wa ukatili aliofanyiwa kwenye jamii.

Mwalimu wa Malezi wa Sekondari Lunguya, John Banda, anasema wameanzisha dawati la malezi, unasihi, ulinzi na usalama kwa wanafunzi, litakalokuwa na jukumu la kusikiliza kero mbalimbali zinazowakabili ndani ya eneo la shule na kwenye jamii na kuzitatua ili wasikimbie masomo na kushindwa kutimiza ndoto zao.

Ofisa mtendaji wa kata ya Shilela, Mwanaidi Mzee, anawataka wazazi na walezi kuwafichua watu wanaofanya ukatili wa kijinsia kwa watoto kwenye ngazi za familia ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuacha tabia ya kuingia makubaliano watu wanaobainika kuwapa mimba wanafunzi.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhitaji, anawataka watoa huduma kwenye kituo hicho kutojihusisha katika vitendo vya rushwa wakati wa utoaji wa haki kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia na badala yake wafanye kazi kwa kuzingatia miongozo na kuwa wasiri pale wanapopatiwa taarifa.

Aidha, anasema serikali kwa kushirikiana na wadau wanatenga fedha kwa ajili ya kutatua changamoto zinazowakabili wananchi hasa katika masuala ya afya, elimu na matukio ya ukatili, hivyo watalaamu wa afya na jeshi la polisi wahakikisha wanayatumia majengo hayo katika kutoa huduma stahiki.

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

# Ndivyo wachafuzi wakubwa mazingira kama hawa wanavyoendelea kuitesa Afrika



Mitambo ya mafuta ya ARAMCO huko Jeddah, Saudi Arabia mwaka 2021. **PICHA: AP**

WAAFRIKA wanakutana jijini Nairobi Kenya kwenye 'Africa Climate Summit' 2023, mkutano wa kwanza wa kilele kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi barani Afrika.

Ni kwa siku tatu, viongozi wa Afrika watajadili na wataalamu wa mazingira, wanasayansi, wadau mashirika ya kiraia pamoja na kampuni za umma na binafsi pamoja na mashirika ya kimataifa, mustakabali wa bara hilo kwenye athari za uharibifu wa mazingira.

Lengo ni kuafikiana kwenye mtazamo mmoja wa Afrika ili kupata msimamo wa kuuwasilisha kwenye mkutano mwingine wa utakaofanyika Desemba huko Dubai Falme za Kiarabu.

Kwa mujibu wa RFI wakati huu, washiriki wanataka vitendo. "Hakuna suala la kukutana bila matokeo yoyote chanya, kama inavyokuwa mara nyingi wakati wa mikutano kama hiyo,"

Takribani viongozi 20 wa nchi na serikali za Afrika na karibu wajumbe 20,000 kutoka duniani kote wanakutana Nairobi, inasema RFI. Wakati wa mkutano huo Afrika inabaki kuumizwa na ukweli kuwa haichangii uharibifu wa mazingira na uchafu wa hali ya hewa duniani lakini ni mwathirika mkubwa.

Kwa mujibu wa Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Mazingira UNEP, Afrika kwa ujumla inachangia chini ya asilimia tatu ya jumla au kiwango cha hewa chafu duniani.

Lakini, ni mwathirika zaidi, mathalani, nchi za Kusini ya Sahara zinategemea kwa asilimia 95 kilimo cha mvua, ambacho ndicho kinachoajiri mamilioni ya raia, ndilo tegemeo pato la taifa na chakula, hivyo uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi huongeza hatari na athari zaidi kwao.

Kwenye kilimo na ufugaji, wanyama na nyuki, wakati wote kunatetereka. Mabadiliko huleta ukame, uhaba wa maji, kukosa malisho wakati mito na maziwa hukauka na bahari kuongezeka kina na joto yote huathiri uvuvi.

Kwa ujumla huongeza umaskini, njaa, upotevu wa mapato, magonjwa na udhaifu wa watu na uchumi kitaifa kila wakati, kwa hiyo Afrika inakuwa mwathiriwa mkubwa wa majanga ya mabadiliko ya hali ya hewa kutokana na umaskini, uduni kiuchumi na kukosa teknolojia.

Mathalani, hivi karibuni wataalamu wa Umoja wa Mataifa (UN) wanailaumu kampuni kubwa ya mafuta ya Saudia ya ARAMCO, kutokana na kazi zake kuchafua mazingira duniani.

Ni katika barua zilizotangazwa hadharani wiki iliyopita Agosti 26 mwaka huu, zikisema kampuni kubwa ya mafuta ya Saudi Arabia madhara yake kwenye ongezeko la joto duniani yanatisha, inasema Redio ya RFI.

Kwa mujibu wa barua hizo, nishati ya mafuta inahusika kwa zaidi ya asilimia 75 ya uzalishaji wa gesi chafu duniani. Zinataja ripoti zinazokadiria kuwa zaidi ya nusu ya uzalishaji huu unaweza kuhusishwa na makampuni 25 katika sekta ya mafuta ,

Wakati huo "Saudi Aramco ikitajwa kuwa ni msambazaji mkubwa zaidi wa gesi zinazochafua mazingira".

"Kwa hiyo, kutokana na uzalishaji wake wa kihistoria, Saudi ARAMCO ingekuwa tayari imechangia kwa kiasi kikubwa athari mbaya za haki za binadamu zinazohusiana na mabadiliko ya tabinchi."

Wataalamu wa UN ni watu huru, wasio na malipo ambao hawazungumzi kwa niaba ya Umoja wa Mataifa, lakini wanawajibika kuripoti matokeo yao kwa umoja huo. Barua hiyo imeitaka kampuni hiyo kutoa maoni yake kuhusu hoja 10 ndani ya siku 60.

Hata hivyo RFI inasema hakuna jibu kutoka kwa walalamikiwa lililoonekana kwenye tovuti ya UN.

Inaelezwa kuwa faida ya ARAMCO ndiyo chanzo kikuu cha ufadhili wa mpango mkubwa wa mageuzi ya kiuchumi na kijamii, yenye lengo la kuwezesha ufalme wa Saudia kuleta mseto wa uchumi wake, ambao kwa kiasi kikubwa unategemea nishati ya mafuta.

Saudi ARAMCO ndilo kampuni mzalishaji mkubwa wa mafuta duniani. Kampuni hiyo inayojulikana rasmi kama Kampuni ya Mafuta ya Saudi Arabia, inamilikiwa na serikali na iko Dhahran, Saudi Arabia.

Inaelezwa kuwa ni kampuni yenye faida kubwa zaidi duniani, ikipita kwa mbali kampuni kubwa za kiteknolojia kama vile Apple (AAPL) na Google ya Alphabet (GOOGL) na kwamba mwana hisa mkuu ni serikali ya Saudi Arabia.

ARAMCO inafanyabiashara jijini London ikiwa na kampuni tanzu ya Aramco Trading Limited (ATL), ambayo itaendesha shughuli za biashara barani Ulaya na kupanua wigo wa utendaji hadi kufikia Afrika Kaskazini na Magharibi pia.

Mambo kama hayo ni changamoto zaidi kwa Afrika kwa kuwa haiwezi kuhimili wala kukabiliana na changamoto kama hizo na kuendelea kuumia.

# Mtaalamu atoboa siri kubomoka familia, utandawazi kunavyoumiza

**INATOKA UK.11**

Mwenyekiti wa Bodi ya YPC Martine Mng'ong'o, akizungumza na washiriki wa jukwaa hilo, anasema kwasasa ni vizuri wazazi na walezi wakabadilika kwenye malezi ya vijana wao ili baadae wasije wakaenda kinyume na maadili kwani kwasasa wengi wanajifunza mambo mengi kupitia teknolojia tofauti na ilivyokuwa zamani.

Mng'ong'o anasema YPC iligundua kuwepo kwa mabadiliko kwa vijana kupitia teknolojia jambo ambalo limewasukuma kutoa elimu hiyo kwa vijana na wazazi kupitia Jukwaa hilo ambalo linafanyika kila mwisho wa mwezi.Mwalimu Amina Kijuu, kutoka Shule ya Msingi Kambarage iliyopo Kibaha , anasisitiza mabadiliko ya malezi kwa wazazi ili kuwanusuru vijana kufanya vitu ambavyo ni tofauti na maadili yao.

Amina anaeleza kwamba hali ya maadili kwa watoto imebadilika tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo amesisitiza wazazi kuwalea watoto kiimani jambo ambalo litakuwa msaada kusimamia imani zao.

"Tuwasisitize watoto kuishi kwenye imani zao, tuwakazanie kushiriki ibada na kufuata mafundisho ya kiimani na hii itawasaidia kuwa na hofu ya Mungu. Vingine kizazi kinaweza kukengeuka" anasema Amina.

Mwalimu huyo pia anaeleza kwamba endapo wazazi watasimama kwenye nafasi zao na kuwa karibu na watoto itapunguza vitendo vya ukatili ikiwemo ubakaji na ulawiti kwa watoto ambao kwasasa umeshamiri kwenye maeneo mbalimbali.

Katika karne zilizopita utaratibu wa bibi kuwasimulia wajukuu hadithi ambazo kwa namna moja au nyingine zilikuwa na mafundisho ambayo yalishi kwa watoto na walikuwa wakiyafuata tofauti na siku hizi.

Karne hii ya 21 ina mabadiliko makubwa watoto wanajikita kuangalia katuni na tamthilia zinazoonyeshwa kwenye runinga, simu na kwenye vibanda umiza wanajifunza mambo mengi yanayohusiana na ngono.



# Utafiti waonyesha kiwango nguvu kazi chaongezeka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa matokeo ya utafiti wa nguvu kazi uliofanyika mwaka 2020/21 unaonesha kiwango cha ujuzi cha juu kimeboreka huku cha kati kikiongezeka kutoka asilimia 16.6 mwaka 2014 hadi 19.9 mwaka 2021.

Mafanikio hayo yametokana na kutekelezwa kwa programu za vijana ikiwamo Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi.

Hata hivyo, serikali imepanga kufanya tathmini mahususi ya mafunzo yanayotolewa kupitia programu za kuwezesha vijana mwaka 2024/25 ili kubaini mafanikio yaliyopatikana na kuwawezesha vijana.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Ng'wasi Kamani.

Alihoji, ni lini serikali itatumia mfumo gani kuhakiki ubora na matokeo chanya ya programu mbalimbali zinazotolewa kwa vijana.

Katambi alisema kiwango cha ujuzi wa chini kimepungua kutoka asilimia 79.9 mwaka 2014 hadi 76.9 mwaka 2021.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kusimamia utekelezaji wa programu hizo ili ziweze kuleta tija kwa taifa, sambamba na hatua hiyo, mwaka wa fedha 2024/25, serikali imepanga kufanya tathmini mahususi ya mafunzo yanayotolewa kupitia programu mbalimbali za kuwezesha vijana ili kubaini mafanikio yaliyopatikana na kuwawezesha vijana kujiajiri au kuajirika," alisema.

Awali, alisema serikali imeweka Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Miradi na Programu zote zinazotekelezwa ikiwamo za vijana.

"Katika kutekeleza hilo mwezi Januari, 2022 serikali ilitoa Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Miradi na Programu za Maendeleo."

"Kwa kuzingatia mwongozo huo, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu mbalimbali kila robo mwaka," alisema.

Aidha, alisema Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu imekuwa ikifanya tafiti ili kupima matokeo ya utekelezaji wa programu mbalimbali, ikiwamo utafiti wa nguvu kazi ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema kumekuwa na tatizo vijana wengi wanaonufaika na program hizo kushindwa kuunganishwa moja kwa moja na masoko ya ajira na mitaji wanapohitimu.

"Nini mkakati wa serikali wa kuhakikisha vijana hawa wanapohitimu wanaunganishwa na program hizi pamoja na masoko ya ajira na mitaji wasirudi mitaani ili kutoondoa tija ya programu wanazopata," alihoji.

Katambi akijibu maswali hayo, alisema kupitia Halmashauri wapo Maofisa Maendeleo ya Vijana na Jamii wanaendelea kutoa mafunzo kwa utaratibu wa mwongozo na mikopo ya asilimia 10 hutangazwa na hutolewa.



Mjumbe wa mkutano mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Dodoma, Bashiru Iddi, ambaye pia ni Mwenyekiti wa chama hicho Kata ya Chang'ombe, akizungumza na wananchi kwenye mkutano uliofanyika jana baada ya kufanya ziara ya ukaguaji na utekelezaji wa ilani ya CCM katika matawi 6 na mitaa7 yaliyopo Jiji la Dodoma.**PICHA: PETER MKWAVILA**

# Bil. 11/- zalipwa wananchi kuathiriwa wanyamapori

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii imesema ndani ya miaka 10 ya kutumika kwa kanuni za kifuta jasho na machozi Sh. bilioni 11.3 zimelipwa kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu.

Hata hivyo, serikali ipo kwenye hatua za mwisho za kufanyia marekebisho kanuni hizo ili wananchi wapate malipo yanayoendana na uharibifu uliofanywa na wanyama hao.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dastan Kitandula, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti maalum (CCM) Yustina Rahhi.

Alihoji serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mfuko wa fidia kwa waathirika wa madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Naibu Waziri Kitandula alisema serikali imekuwa ikilipa kifuta jasho na kifuta machozi kama mkono wa pole au faraja kwa wananchi wanaopata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu.

"Malipo hayo yamekuwa yakifanyika kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho na Machozi za mwaka 2011 na kwa kadri ya upatikanaji wa fedha," alisema.

Kadhalika, kanuni hizo zilianza kutekelezwa mwaka 2012 na katika kipindi cha kuanzia 2012/2013 hadi 2022/2023, Sh. bilioni 11.3 zimelipwa kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu.

Alisema suala hilo limekuwa ni tatizo kubwa kwa nchi nyingi za Afrika na limesababisha baadhi ya nchi kuondokana na utaratibu wa kulipa kifuta jasho na machozi, lakini Tanzania imeendelea kuona umuhimu wa kuwafuta jasho na machozi wananchi kwa madhara wanayoyapata kutokana na wanyamapori hao.

# Mwongozo upatikanaji sawa huduma kijinsia waandaliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema ili kuhakikisha kuna uwiano wa kijinsia katika upatikanaji wa huduma imeandaa mwongozo wa uwiano wa kijinsia unaoshirikisha makundi yote kwenye maendeleo ya jamii na kuondoa ukatili.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na Maofisa Ustawi wa Jamii wa wizara za kisekta, taasisi za umma na wadau kwenye mafunzo ya utoaji wa huduma kwa kuzingatia uwiano wa kijinsia ili kufikia kizazi cha usawa jijini hapa.

"Mwongozo huu umelenga kutekeleza makubaliano ambayo Tanzania imeridhia katika mikataba yake ya kimataifa lakini pia katiba yetu ya Tanzania inaelekeza kutoa huduma kwa watu wote bila ubaguzi wowote," alisema Mpanju.

Alisisitiza Maofisa Ustawi hao kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika mafunzo hayo ili maarifa yote yanayopatikana yatumike nchi nzima ili lengo la serikali kuwa na jamii yenye usawa litimie.

Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Nandera Mhando, alisema mwongozo huo umeandaliwa kupitia hatua kadhaa ikiwamo vikao na kufanyiwa majaribio na wadau na kupitia mafunzo mbalimbali hadi kufikia hatua ya ukamilishaji.

"Malengo ya semina hii ni kutoa uenezi wa mwongozo huu kwa maofisa ustawi ili utumike nchi nzima na kuzibe mapengo yote yaliyokuwapo kwenye uwiano wa kijinsia nchi nzima," alisema Dk. Nandera.

Mkurugenzi Msaidizi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Subisya Kabuje, alisema mwongozo huo utafanikiwa zaidi endapo utasambazwa kwa maofisa ustawi wote kutoka mikoa na halmashauri zote na kusaidia kutatua kero.

Mwakilishi kutoka Shirika la PACT Tanzania, Flora Nyagawa, alisema shirika hilo litaendelea kushirikiana kikamilifu na wizara kuhakikisha hatua zote zinatekelezwa ili kuwa na taifa lenye uwiano wa jinsia.





# Wanafunzi walilia umeme kujisomea usiku

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Madilu, wilayani Ludewa mkoani Njombe wamelalamikia kukosekana kwa umeme shuleni hapo huku nyumba za starehe ukipatikana.

Wakizungumza na Nipashe, walisema inaumiza kuona maeneo ya starehe umeme unapatikana na kulazimika kutumia umeme wa jua ambao hauwaki kwa muda mrefu kwa sababu ya hali ya hewa ya baridi.

Mmoja wa wanafunzi hao, Exavery Erick, alisema kukosekana kwa nishati hiyo ni tatizo kubwa kwa wanafunzi.

"Kwa sisi wanafunzi inatuathiri kwa sababu unapokuwa unasoma ule mwanga ambao unatoka kwenye solar unaumiza sana macho, wanafunzi wengi wanaumwa macho wanatumia miwani kitu ambacho siyo kizuri kwa hiyo hii ni changamoto kubwa pia mtu anakosa hamu ya kusoma kwa sababu ukiingia darasani unakutana na hizi solar ambazo ukikaa kwa saa tatu zinazima,," alililamika.

Wameiomba serikali kuwaletea nishati ya umeme kwa sababu nguzo hazipo mbali.

"Nguzo zipo kama kilometa mbili au moja, umeme umekuwa ukitumika huko mitaani kwenye baa kwenye gesti na sio hapa kwenye taasisi muhimu kama hii, tunaumia," alisema Erick.

Kaka mkuu, Musa Mwang'ombe alisema suala la umeme ni changamoto kubwa."Tunavyojua solar inahitaji hadi kuwapo kwa jua, lisipokuwapo basi solar hazina msaada wowote kwa hiyo kutokana na changamoto hii wanafunzi tunashindwa kusoma vizuri hasa usiku," alisema.

Dada mkuu, Magret Mlelwa, alisema kukosekana umeme shuleni hapo kunasababisha wanafunzi kushindwa kusoma vizuri.

Mwalimu mkuu shule wa sekondari hiyo, Michael Mwalongo, alisema changamoto ya kukosekana kwa umeme ilitokana na wakati wanapitisha miundombinu ya nguzo za umeme eneo hilo lilirukwa.

"Baada ya kurukwa sisi tuliwahoji maswali kwanini huku sekondari nguzo za umeme hazipiti mnapitisha maeneo mengine wakati taasisi ndiyo eneo la kwanza kabisa kufikiriwa, lakini wakasema tutaleta kwa awamu ya pili lakini nayo ikapita kwa hiyo tukaendelea kupaza sauti kwa viongozi ndani ya kata, wilaya na ngazi ya mkoa hatujafika kwa sababu bado tunao viongozi.Tumefanya jitihada kuandika barua kwa Tanesco wilaya tumeahidiwa lakini bado," alisema Mwalongo.

Ofisa Elimu Sekondari, Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Michael Hadu, amekiri kuwapo kwa changamoto hiyo.

"Tunatumia umeme wa solar ambao hauna nguvu kutokana na hali hiyo ukosefu wa umeme shule hii imekuwa haifanyi vizuri katika mitihani ya kitaifa, mwaka jana ilikuwa kati ya shule tatu duni za mkoa wa Njombe na tulipofuatilia programu ya KPI tumebaini kinachochangia zaidi ni ukosefu wa mwanga umeme," alisema Hadu.

Alisema kwa mujibu wa serikali ilielekeza eneo lisilokuwa na umeme, unafika lakini Kijiji cha Madilu umeme upo shuleni hakuna.

"Tunaendelea kuomba wanaohusika hususani Tanesco watuletee umeme kwenye shule yetu ya Madilu kwa sababu ni changamoto ambayo tunaiona inarudisha nyuma maendeleo ya taaluma lakini hata walimu tukiwapangia huku hawaifurahii sana shule hii kwa sababu inakosa miundombinu ya umeme," alisema Hadu.

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Ludewa, Yusuph Sukwa, alisema kata ya Madilu haihudumiwi na Tanesco bali inahudumiwa na muwekezaji ambaye ni mzalishaji wa umeme Madope Hydro Power company.

Nipashe ilimtafuta meneja wa mradi wa Madope Hydro company, Injinia Kulwa Masanja, ambaye alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo na kwamba tayari bajeti imeshatengwa kwa ajili ya kupeleka umeme shuleni hapo.



Farida Abdallah, Mwanachama wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Mabwepande akichangia hoja kwenye kikao cha kujadili mbinu za kuwezesha wanawake kushiriki katika ngazi mbalimbali za uongozi, kilichofanyika Bunju B, Dar es Salaam juzi. **PICHA SABATO KASIKA**

## Polisi yafungua dirisha jipya kusalimisha silaha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limefungua dirisha jipya la wananchi wanaomiliki silaha haramu kuzisalimisha kwa hiari huku likisisitiza kuendesha operesheni maalumu ya kuzisaka baada ya muda uliopangwa kwisha.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, aliyasema hayo juzi alipozungumza na wandishi wa habari kuhusu operesheni mbalimbali zinazofanywa na jeshi hilo.

Alisema dirisha la usalimishaji wa silaha hizo lilifunguliwa Septemba mosi, mwaka huu na litafungwa Oktoba 31 na kuwataka wananchi wanaomiliki silaha hizo kusalimisha kabla ya muda huo.

Vile vile, zinatakiwa kusalimishwa kwenye vituo vya polisi vilivyo jirani, ofisi za serikali kuanzia serikali za mitaa, kata, tarafa na wilaya.

"Mwananchi yeyote ambaye atasalimisha silaha haramu kwa kipindi hiki cha miezi miwili hatakamatwa wala kuchukuliwa hatua zozote za kisheria, usalimishaji wa silaha hizi utafanyika kuanzi saa 2:00 asubuhi mpaka saa 10:00 jioni," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema baada ya miezi miwili iliyopangwa kuisha jeshi hilo litaanza kufanya operesheni maalumu ya kusaka na kuwachukulia hatua wale wote watakaokutwa wakimiliki silaha hizo.

# Jukwaa la Wanawake Vijijini laanzishwa Nyanda Juu Kusini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JUKWAA la Wanawake wa Vijijini tawi la Tanzania limeanzishwa nchini kupitia Mkutano Mkuu wa kwanza wa jukwaa hilo uliowashirikisha washiriki 50 kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Kupitia mkutano huo viongozi mbalimbali walichaguliwa na kupewa kazi ya kuliendesha kwa kipindi cha mwaka mmoja huku Vailet Mkoma, kutoka wilayani Mbozi mkoani Songwe akichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kitaifa na Aksa Kauzeni kutoka Sumbawanga mkoani Rukwa, akachaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti.

Pia, Eloy Satulo kutoka wilayani Mbarali, mkoani Mbeya alichaguliwa kuwa katibu mkuu wa kitaifa na Felista Madembwe alichaguliwa nafasi ya makamu mwenyekiti, Mainala Kalinga kutoka Mbozi alichaguliwa nafasi ya mtunza fedha na Flora Mlowezi, afisa habari wa Jukwaa.

Akifungua mkutano huo uliofanyika katika Halmashauri ya Mbeya vijijini, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali la MIICO lililoratibu kuanzishwa kwa Jukwaa hilo nchini, Catherine Mulaga, alisema linalenga kuwafanya wanawake kujikita katika agenda kuu muhimu za ardhi, kilimo ikolojia, ukatili wa kijinsia na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mulaga alisema jukwaa ambalo kwa mataifa mengine yalipo ukanda wa SADC lilikwisha anzisha linaamini kupitia agenda hizo wanawake watajadiliana kwa pamoja na kuwa na mchango katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizopo kwenye maeneo hayo ikiwamo wao wenyewe kumiliki ardhi.

"Katika suala la ardhi bado kuna changamoto ya wanawake kutopewa nafasi ya kuwa sehemu ya wamiliki kama ilivyo kwa wanaume.

Lakini tunapozungumzia kilimo ikolojia tunataka mwanamke awe sehemu ya watumiaji wa mbegu bora, utunzaji wa mazingira na mwenye kujua athari za mabadiliko ya tabia ya nchi," alisema Mulaga.

"Suala la ukatili wa kijinsia bado ni changamoto kwenye jamii zetu hasa kwa wanawake wanaoishi maeneo ya vijijini ambao licha ya kuwa na ushiriki mkubwa kwenye uzalishaji mali ikiwamo kupitia kilimo bado hawapewi nafasi ya kufanya maamuzi," aliongeza.

Alisisitiza jukwaa hilo kuwapa nafasi wanawake wadogo (mabinti) akisema kuwapo kwao kwenye majukwaa kama hayo kunawapa uzoefu na kuwezesha maarifa yanayopatikana kuwa endelevu huku pia akisema wanayo mambo mapya wanayoweza kuyaongeza kwa watu wazima.

Aliwasihi wanawake pamoja na kuwa na majukwaa yao kutowatenga wanaume kwenye masuala mbalimbali wanayojadili sambamba na wasaidizi wa masuala ya kisheria kwa kuwa ushirikiano wa pamoja utawezesha uelewa wa pamoja wa makundi hayo na kuifanya jamii kupiga hatua zaidi.

Mwenyekiti, Vaileth Mkoma, aliwasihi wanawake waliopata bahati ya kuwa waanzilishi wa jukwaa hilo kwenda kuwa mfano wa kuigwa kwa wenzao waliopo vijijini ili baada ya kuwapo kwa jukwaa ngazi ya taifa yaanzishwe kwenye ngazi za mikoa, wilaya, kata na vijiji.

HABARI KITAIFA

# Vituo vyafungiwa kwa kuficha mafuta

**Na Waandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imefungia vituo vitatu kati ya miezi sita na muda usiojulikana kwa kosa la kuficha mafuta.

Mamlaka hiyo imesema inawachunguza wafanyabiashara 16 kwa kuhodhi mafuta na wakikutwa na kosa hilo adhabu yake ni kushtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, akizungumza na waandishi wa habari jana alisema, kuna mafuta ya kutosha nchini, lakini baadhi ya wafanyabiashara wanaficha.

"Pamoja na kuwapo kwa mafuta, baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakichukua mafuta na kuchelewesha kufikisha vituoni huku wengine wakiwa na mafuta kwenye visima, lakini hawauzi ikiwamo Kampuni ya GBP," alisema.

Alisema, kutokana na hali hiyo waliamua kufunga kituo hicho kilichopo mkoani Tabora kwa muda na EWURA itavifungia vituo vingine endapo havitauza mafuta.

"Iwapo hawatatoa utetezi unaojitosheleza kituo hicho kinaweza kufungiwa kwa kipindi cha miezi sita," alisema.

Dk. Andilile alisema EWURA imefungia kituo cha mafuta cha Camel Oil cha Msamvu na Matemba cha Turiani, mkoani Morogoro kwa miezi sita.

"EWURA imejiridhisha kuwa nchi ina mafuta ya kutosha kwani kuna mafuta kwenye maghala na mengine ambayo yako kwenye meli zilizowasili bandarini zikisubiri nafasi ya kuingia kwenye gati na kuyashusha," alisema.

Dk. Andilile alisema meli ya MT. Ellie Lady ina lita milioni 58.06 za dizeli kwa ajili ya matumizi ambayo iliwasili Agosti 29, mwaka huu imeanza kushusha Septemba 3 na inatarajia kumaliza kushusha Septemba 10.

Alisema meli ya MT Emma Grace ina lita milioni 17.23 za petroli iliwasili Agosti 29, mwaka huu, inatarajiwa kuanza kushusha Septemba 8 na kukamilisha Septemba 12 mwaka huu.

"Meli ya MT High Tide ina lita 22,302,452 za petroli kwa ajili ya matumizi hapa nchini iliwasili Agosti 28 itaanza kushusha mafuta Septemba 12 na kukamilisha Septemba 16 mwaka huu," alisema Dk. Andilile.

Dk. Andilile alisema kwa mafuta yaliyopo katika maghala na yale yaliyopo kwenye meli zilizowasili, nchi ina mafuta yatakayokidhi mahitaji ya siku 19.

Aidha, alisema kutokana na changamoto za kidunia na siasa wamejikuta wameathiriwa kutokana na benki ya Marekani kubadili sera zake za fedha ambayo kwa sasa imesababisha viwango vya riba kutoka asilimia 2.5 Novemba, mwaka jana mpaka asilimia tano Mei, 2023.

Alisema ukwasi wa Dola ya Marekani kwenye soko la dunia unapungua kwa sababu watu wanachukua dola kokote na kuwekeza Marekani kwa sababu wanajua watapata faida kubwa ya asilimia tano.

**HALI ILIVYO**

Mjini Tabora baadhi ya vituo vya mafuta havikuwa na nishati hiyo kwenye maeneo yenye huduma hiyo huku wananchi wakiomba serikali kuingilia kati.

Mwendesha bodaboda Juma Ally alisema lita moja ya petroli ni Sh.3,307 bei elekezi ya serikali na wanakesha vituoni kusubiri mgao bila mafanikio.

Mjini Njombe wananchi walionekana kwenye foleni kutafuta mafuta hali iliyosababisha nauli kupanda kutoka Sh. 500 hadi 1,000 kwa bajaj na 1,000 hadi 2,000 kwa bodaboda.

John Njiuka, alisema madhara ya kukosekana kwa mafuta ni makubwa kwa wajasiriamali kwa sababu inawalazimu kukaa kuanzia asubuhi hadi jioni kusubiri, lakini wanaambiwa hakuna. Alfred Mlelwa alisema amesafiri kutoka kijijini umbali wa kilometa 45 kufuata mafuta mjini baada ya kuuziwa Sh.4,000 kwa lita moja.

Katibu Tawala wilaya ya Njombe, Agatha Mhaiki alisema wamefanya ukaguzi na kubaini mafuta hakuna.

Eneo la Bagamoyo waendesha bodaboda na bajaji walilazimika kupandisha bei ya kusafirisha abiria kutoka eneo moja hadi jingine wakidai ni uhaba wa mafuta.

Mkoani Kilimanjaro tatizo la kukosekana mafuta hayo katika baadhi ya vituo vya katikati ya miji, limemshtua Mkuu wa mkoa huo, Nurdin Babu, ambaye licha ya kukiri kushuhudia makali hayo jana (juzi), ameonya wafanyabiashara wanaoficha mafuta ili kusubiri yapande bei.



Mwenyekiti wa Mtandao wa Kutokomeza Ukeketaji Tanzania, Roman Selesini, akizungumza kwenye kikao cha wanachama wa mtandao huo cha kuweka mikakati ya kukabiliana na ukatili huo, kilichofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Rais Mwinyi ataka taifa lilindwe kudhibiti mmomonyoko maadili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewasihi waumini wa dini, wazazi na walezi kwenye jamii kuhimiza maadili mema kwenye malezi ya vijana wao ili kulinusuru taifa na athari za mmomonyoko wa maadili.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo huko Kidoti Mkoa wa Kaskazini Unguja alikoshiriki dua ya kuliombea taifa na viongozi wake.

Alisema malezi bora kwa jamii yanayoendana na mila, sila na tamaduni za asili ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla yanayotokana na misingi ya dini ili kulinusuru taifa na athari za dawa za kulenya, udhalilishaji, wizi, uzembe, kubaguana na vijana waliokosa hofu ya kumwogopa Mwenyezi Mungu.

Pia, alisifu hali ya amani, umoja, mshikamano na maelewano iliyopo nchini na kuitaka jamii kuendelea kuitunza, pia alihimiza udugu na umoja bila kujali tofauti zao za kisiasa kwa kutekeleza shughuli za kijamii na kimaendeleo.

"Ndugu zangu kila mara nasema na leo napenda nirudie tena katika mambo muhimu katika nchi yoyote, amani ni jambo la msingi na la kupewa umuhimu wa kipekee, nchi ikikosa amani hakuna jambo lolote linaweza kufanyika," alisisitiza.

Aliahidi kutimiza ahadi zote alizoziweka wakati uchaguzi mkuu wa Zanzibar kwa wananchi pamoja na kuyatekeleza mambo muhimu yaliyokuwa hayako kwenye ahadi zake nakueleza ni wajibu kwa viongozi kuyatekeleza kwa maslahi ya watu na taifa kwa ujumla.

Dua hiyo ya kuliombea taifa ilizishirikisha zaidi ya madrasa 700, viongozi wakuu wa dini, serikali pamoja na vyama vya siasa.

# ACT Wazalendo yataka wazawa waendeshe Bandari na DP World

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimependekeza kampuni maalum ya wazawa itakayoingia ubia na DP World kushirikiana kuendesha shughuli za miradi katika eneo la bandari.

Akitoa tamko rasmi la chama hicho kuhusu makubaliano ya IGA (Intergovernmental Agreement) kati ya Tanzania na Serikali Dubai.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Tanzania Bara, Dorothy Temu, alipendekeza hayo jana alipotangaza msimamo wa chama hicho kuhusu sakata la Bandari, kwa waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho Magomeni, Dar es Salaam.

Alisema chama chao hakipingi hoja ya serikali kuhusu uendelezaji wa Bandari nchini, lakini kinataka mkataba ufanyiwe maboresho.

Dorothy alisema mapendekezo yao yametokana na kamati maalum iliyoundwa na Kiongozi wa Chama chao, Zitto Kabwe, ikioongozwa na timu ya wataalamu 22 wakiwamo Wakili Emmanuel Mvula na Msemaji wa Kisekta wa Mipango, Uwekezaji na Hifadhi ya Jamii. Walifanyia kazi masuala yaliyoibuliwa kuhusu makubaliano hayo na kutoa mapendekezo kwa uongozi wa chama na Taifa.

"Ubia utakaopendekezwa uwe ni wa kampuni maalum ya umma kumiliki mpaka asilimia 50 ya hisa zote za Kampuni ya Ubia.

"Ardhi ya Bandari ya Dar es Salaam katika gati husika, uwekezaji ambao umeshafanywa na serikali uwe sehemu ya mchango kupata hisa ambazo serikali itazimiliki katika Kampuni ya Ubia.

"Serikali iweke mazingira ya kisheria na mfumo wa kimkataba utakaoruhusu ushiriki wa ndani kuwa wa mara moja au kupitia mfumo wa Kampuni ya DP World, kuwekeza na baadaye sehemu ya hisa kununuliwa na wawekezaji wa ndani kwa kadri watavyokuwa na uwezo hadi kufikia ukomo wa fursa za wawekezaji wa ndani.

"Muda wa Usuluhishi upunguzwe, na hatua za usuluhishi zisizidi siku 45. Hii ni kwa sababu bandari ndiyo chanzo kikuu cha mapato nchini. Mapato yote yatakayopatikana wakati kesi ikiendelea, inapendekezwa yawekwe kwenye akaunti maalum hadi pale kesi itakapomalizika na uamuzi kutolewa," alisema.

Dorothy alisema kuwa uchambuzi wao umebaini IGA kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai haikuboreshwa bungeni wakati wa kuridhia Azimio la Bunge. Sababu kubwa wanaona ni Bunge kuwa na wabunge wengi wa chama kimoja.

"Ni muhimu kwa ACT Wazalendo kuendelea kushirikiana na wadau wengine wa demokrasia kupigania kupatikana kwa Katiba Mpya na Tume Huru ya Uchaguzi ili wananchi wapate Bunge linalotoa taswira halisi ya mfumo wa vyama vingi vya siasa litakaloweza kusimamia maslahi ya nchi kwa weledi na ukamilifu wake.

"ACT Wazalendo inawataka wanachama wake kuendelea kutoa shinikizo kwa serikali kutekeleza ahadi yake na matakwa ya wananchi kukwamua Mchakato wa Katiba Mpya na mageuzi ya kisiasa kwa kupeleka bungeni Muswada wa Sheria ya Uchaguzi unaoanzisha Tume huru ya Uchaguzi, Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa kuweka uwanja sawa wa vyama vya siasa kufanya siasa, muswada wa marekebisho madogo ya vifungu vya Katiba (minimum reforms) kuwezesha sheria mpya za uchaguzi na muswada wa marekebisho ya kuanzisha/kuendeleza mchakato wa Katiba Mpya," alisema.

***Imeandaliwa na Halfani Chusi na Neema Msalaba (UDSM)**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**TAYANAN PHESTOR LUKIKO** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE 123655** iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM PCO mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kitu chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: ***WMB/RB/104/2023***

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**TEDDY JUSTINE NTIMA** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 201534** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 26/9/2019. Tarehe ya kuisha matumizi ni 25/9/2029. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU/4460/2023.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya .SENGEREMA**

**Kituo Cha NYAHUNGE ................Mkoa wa. MWANZA**

**Shauri/ ndoa Na 20/ 2023**

**Jina la Mdai MARY NABUNJE CHRISTOPHER**

**Jina Mdaiwa GWAMAKA BENSON MWAMLENGA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za uratibu madai katika mahakama ya mwanzo kwa)**

**GWAMAKA BENSON MWAMLENGA MKAZI WA KALIUA- TABORA SIMU NO 0623 945161**

Kwa kuwa mdai/wadai wameleta madai yao/yake kwamba(eleza hapa habari za madai **(KUOMBA TALAKA, MATUNZO YA WATOTO WAWILI TSH 300,000/= KILA MWEZI NA MGAWANYO WA MALI YA NDOA.** Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 07 mwezi 09 mwaka 2023 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini. Mahakama inaweza kusikiliza shauri hilo bila ya wewe kuwepo

Hati hii imetolewa kwa Amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe **04 mwezi 09 mwaka 2023.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**

**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 100 of 2023**

**In the Matter of the Estate of the late ANTHONY KIPEJA BULOGWA of mwaja chinangali within Dodoma region**

**AND**

**In the matter of application for letters of administration by ANNA MARCUS NGWANDO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 13 day of 09......................... 2023

**Dated at Dodoma this 10 day of August ..............2023**

PETITIONER

Presented for filing this 23 day of August 2023

RESIDENT MAGISTRATE

**FOMU MIRATH -2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya Moshi**

**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro**

**Usimamizi wa mirathi Na 140 /2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ALISON JOHN HAULE WA MOSHI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUWA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA LAKELO JOHN HAULE**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 Mwezi 09 Mwaka 2023 saa 11:00 asubuhi Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia :**
Endapo kunayeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leo tarehe 23 Mwezi 08 Mwaka 2023

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ASIA ZUBERI MADENGE,** MTAJWA HAPO JUU AMEPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA MAENEO YA BUGURUNI - DAR ES SALAAM YENYE NO: **TAE 128268** ILIYOTOLEWA MAKAO MAKUU UHAMIAJI DAR ES SALAAM MWAKA 2019. TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI KINONDONI NA KUPEWA **RB NO : REF: PHQ/DAR/KIN/7178/2023**

**CHANGE OF NAME BAY DEED POLL.**
**(Cap 117)**
**The Registration of Documents Act.**

BY THIS DEED Made 9TH day of August ,2023 1 **BLANDINA MOSES MOYO** of Postal Office Box number 14 Songea,the name which I was given my parents and name which I have been registered in my Citizen Identify Card with ID NO.19721215 - 57117 - 00001-17 formerly known as **ASHURA MOSES MOYO** the name which I was given after being married appears in my Certificate of Marriage and in my PSSSF documents.

Therefore I do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former name of **ASHURA MOSES MOYO** and assume and determine to take and use the new name of **BLANDINA MOSES MOYO** in substitution of my former name of **ASHURA MOSES MOYO** so relinquished as aforesaid to the intent that I may hereinafter be known not by the aforesaid former name of **ASHURA MOSES MOYO** ,but by the new name of **BLANDINA MOSES MOYO** only.

**AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUIRE** all persons at all times to describe,designate and address me by the new name of **BLANDINA MOSES MOYO.**

**IN WITNESS WHEREOF** I have hereunto subscribed my new name of BLANDINA MOSES MOYO ,and I have affixed my signature the day and year herein after written.

SIGNED and DELIVERED at Songea by the said BLANDINA MOSES MOYO



BEFORE ME:
Name: THERESIA HILMAN MBAWALA
Signature
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**FREDRICK GERSON KISANIFU** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 455 ASC** yenye jina la umiliki **KARAMA IMP & EXP CO. AGENCY.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/7936/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FARES WILFRED TARIMO** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 273 AQP** aina ya **FUSO TIPPER** yenye CHASSIS NO: **FK618D510344.** ENGINE NO: **6D17773535.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/7845/2023.**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0745 700 710.
Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA/KIMATAIFA

# Uganda yazuia shambulizi la bomu kanisani

**KAMPALA,** Uganda

POLISI nchini Uganda wamefanikiwa kuzima shambulizi la bomu lililokuwa lifanywe na mshambuliaji aliyekuwa amebeba kilipuzi akitaka kuingia kanisani katika mji mkuu Kampala.

Polisi nchini humo walisema jana kwamba wamefanikiwa kutibua shambulio la bomu katika kanisa mjini Kampala na kumkamata mwanamume mmoja anayetuhumiwa kwa kujaribu kulipua kilipuzi katika umati wa waumini.

Msemaji wa polisi, Patrick Onyango, alisema mamia ya waumini waliondolewa kutoka Kanisa la Rubaga Miracle Centre katika mji mkuu Kampala baada ya mwanamume kujaribu kuingia katika viwanja vya kanisa hilo akiwa amebeba kilipuzi.

Onyango pia alisema wanawafuatilia wanaume wengine watatu baada ya mshtukiwa huyo mwenye umri wa miaka 28, Ibrahim Kintu, kufichua kwamba huenda alikuwa na watu alioshirikiana nao.

Pia alibainisha kwamba kanisa hilo lilifungwa na watu kuzuiliwa wasiingie, ili kuwapa nafasi maofisa wa kikosi maalumu cha kutengua mabomu na mbwa wa kunusa kufanya upekuzi katika viwanja vya kanisa hilo na kwamba hakukuwa na kitisho zaidi kilichobainika.

Mchungaji wa kanisa hilo, Robert Kayanja, aliliambia shirika la habari la Ufarana AFP kwamba "Bwana amewaokoa kutokana na vifo". **DW**

## Ripoti ya matrekta yaibua mapya

**Na Romana Mallya,** DODOMA

TAARIFA ya Kamati ya Bunge kuhusu mkataba wa mauziano ya matrekta ya Kampuni ya Ursus kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo la (NDC) na wakulima kwa utaratibu wa mikopo imetua kwa Spika, ikitaja athari zilizopatikana kwa wananchi ikiwamo familia kusambaratika.

Athari nyingine ni wananchi kupata hasara kutokana na kuuziwa matrekta yasiyo na ubora au yenye viwango duni na baadhi yao kulazimika kuuza mali zao hivyo kurudisha nyuma juhudi zao za kuondokana na umaskini.

Akisoma jana bungeni jijini hapa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda na Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu changamoto na malalamiko yaliyojitokeza katika kutekeleza mkataba huo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema pia imebainika wapo walioshindwa kulipa madeni hayo.

Spika alisema kuwa Aprili 13, 2023, kwenye kikao cha sita, Mkutano wa 11, Bunge likikuwa na hoja ya serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema wakati wa mjadala kulijitokeza suala la changamoto ya utekelezaji wa mkataba wa ukopeshaji wa matrekta hayo.

"Kutokana na hali hiyo, nilimwagiza Mwenyekiti wa Kamati kukutana na wabunge wa maeneo yaliyokuwa na wananchi walioathirika kwa kiasi kikubwa ili kuwasikiliza na kubaini ukubwa wa tatizo.

"Kamati imekamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa kwangu. Kutokana na changamoto za utekelezaji wa mkataba wa mauziano wa matrekta na kampuni ya Ursus, wakulima wa sehemu mbalimbali waliohusika katika mradi huu waliathirika kwa namna tofauti.

"Wapo waliopata hasara kutokana na kuuziwa matrekta yasiyo na ubora au yenye viwango duni, baadhi yao kuuza mali zao na hivyo kurudisha nyuma juhudi zao za kuondokana na umaskini.

'Wengine waliathirika kiasi cha kuuza mali zao na kuingia kwenye migogoro na familia zao na kusambaratika familia hizo," alisema.

Aliagiza serikali ichambue na kubainisha makundi mbalimbali ya wakulima walioathirika na mradi huo wa kuwakopesha matrekta ya Ursus na kuonyesha namna ya kuwapatia unafuu waathirika hao.




Waandamanaji wakionyesha mabango ishara ya kuwapinga wanajeshi wa Ufaransa kuendelea kuwapo nchini Niger. **PICHA: MTANDAO**

# Waainisha utajiri utakaoachwa nchini

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa kilimo, mifugo na uvuvi nchini wamesema katika siku nne za Jukwaa la Mfumo wa Chakula (AGRF) wanatarajia kupata masoko, kujifunza teknolojia pamoja na wafadhili ili kuboresha shughuli za uzalishaji na uchakataji wa chakula wanazozifanya.

Rais Samia Saluhu Hassan, anafungua mkutano wa Jukwaa leo linalokutanisha wadau zaidi ya 3000 wakiwamo marais kutoka nchi za Afrika, ujumbe kutoka nchi mbalimbali duniani, wataalam, wazalishaji na wachakataji wa chakula kujadili sera mikakati na teknolojia ya kilimo ili kuongeza mnyororo wa thamani wa chakula barani Afrika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Alpha Tanganyika, Flavour Limited, mkoani Rukwa, Alpha Nondo, amesema ni mchakataji wa samaki kutoka Ziwa Victoria na jukwaa hilo ni fursa kwake kutafuta masoko kupitia wadau wa chakula watakao shiriki ili kuongeza wigo wa biashara yake.

Anatarajia kujifunza teknolojia ya ukaushaji wa samaki kutoka kwa wataalamu ili aongeze ubora wa samaki anaokausha wakidhi vigezo vya soko la kimataifa na kunufaika kiuchumi huku akiliingizia taifa fedha za kigeni.

"Baada ya mkutano huo tukae kama wadau wa chakula nchini tujadili ni kitu gani tumejifunza na kuongeza katika uzalishaji wa chakula chetu ili na sisi tuboreshe mnyororo wa thamani wa mazao yetu," alisema.

Alimshukuru Rais Samia kwa kusimamia adhma yake ya kukuza uwekezaji katika maeneo yanayogusa watu wengi ikiwamo chakula na kuleta mkutano huo nchini ili Watanzania wanufaike kuboresha uzalishaji chakula.

Mchakataji wa mboga na viungo kutoka mkoani Arusha, Renalda Mlay, alisema pamoja na kujifunza pia atashiriki kutoa elimu ya uchakati wa chakula wenye viwango na rafiki kwa mazingira ili kupambana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi katika uzalishaji.

Anatarajia kukutana na kushirikiana na wadau wa chakula ili apate ujuzi zaidi kuhusu uchakataji wa viungo wenye viwango vya kukidhi soko la kimataifa na kuitangaza nchi yake.

Meneja mwandamizi, mahusiano na serikali na sera kutoka kampuni ya Sanku, inayojishughulisha na uongezaji wa virutubisho kwenye mahidi, Gwao Omari, alisema kupitia jukwaa hilo anatarajia kukutana na wadau mbalimbali wanaoshughulika na mnyororo wa chakula na kubadilishana mawazo ya kuboresha lishe.

Anatarajia kujifunza kutoka kwa watu wengine wanavyofanya kuboresha lishe kukabiliana na madhara yanayotokana na ukosefu wa lishe kwa jamii ikiwamo utapiamlo, udumavu na vichwa vikubwa.

Pia, kukutana na wafadhili na kuwasaidia katika juhudi za kukabiliana na lishe duni nchini ili waboreshe shughuli zao na kutoa huduma yenye viwango vya juu kwa jamii.

Mkutano huo utampa fursa kujifunza uimarishaji mnyororo wa thamani ya mfumo chakula hasa mahindi ili kuboresha lishe za walaji na namna watakavyoshirikiana kuboresha nafaka hiyo inayotumiwa na watu wengi zaidi barani Afrika.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Kilimo Kusini mwa Afrika (SACAU), Dk. Sinare Yusuph, alisema kupitia mkutano huo watajadili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika uzalishaji wa chakula ikiwamo kilimo, mifugo na uvuvi hasa kwa wazalishaji na wachakataji wadogo.

Mkutano utatoa fursa ya kuwaunganisha wakulima wadogo na katika mfumo wa chakula ikiwamo kuwatafutia soko, kujifunza kutoka kwa wakulima wenzao wanaotoka nje ya nchi ili kuwapa motisha ya kufanya vizuri, kuongeza thamani ya bidhaa zao na kukuza uzalishaji wa chakula nchini.

Mtaalam wa mabadiliko ya tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof Pius Yanda, alisema anatarajia watajadili changamoto za mabadiliko ya tabianchi na kuja na suluhisho la kukabiliana nalo ikiwamo kutumia teknolojia ya umwagiliaji.

Aidha, mikakati ya kikanda ya kukuza mfumo wa chakula, biashara na uwekezaji Afrika Mashariki, kama Tanzania itazalisha chakula iwe na uhakika wa soko katika nchi zinazoizunguka ikiwamo Kenya na Uganda.

Mkurugenzi Idara ya Masoko ya Kilimo na Usalama wa chakula, Wizara ya Kilimo, Dk. Honest Kessy, alisema jukwaa hilo litajadili uboreshaji na ukuzaji mfumo wa chakula ili watu wote wapate vyakula vyenye virutubishi pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa vijana na wanawake kushiriki kwa wingi katika kilimo.

"Kikubwa ni kuhakikisha uzalisaji unaongezeka, vyakula vyenye virutubishi vitazalishwa, gharama za uzalishaji zipungue ili mfumuko wa bei ya chakula usiwe mkubwa kiasi cha kuwanyima Watanzania fursa ya kupata milo mitatu kutokana na mahitaji yao."

Kwa Mujibu wa Dk. Kessy, nchi za Afrika zina changamoto ya uzalishaji zinazosababisha mifumo ya chakula kutokuwa himilivu na kutetereka kunapotokea changamoto kama ilivyokuwa kwenye kipindi cha vita ya Ukraine na Urusi.

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Mjadala mkali kizimbani uhalali umiliki magari ya Bilionea Msuya

**Na Grace Gurisha**

MAGARI manne ya kifahari yaliyodaiwa kuwa yamebadilishwa umiliki kutoka kwa marehemu Erasto Msuya maarufu Bilionea Msuya, kwenda kwa mke wake, Miriam Mrita, hayakuwa na umiliki wa mfanyabiashara huyo na mengine yalibadilishwa umiliki kabla ya kifo chake.

Hayo yalidaiwa jana mahakamani katika kesi ya mauaji ya Dada wa Bilionea Msuya, Aneth Msuya: Namba usajili wa kesi 103 ya mwaka 2018. Washtakiwa ni Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela, wote wakazi wa Mkoa wa Arusha.

Suala hilo la umiliki wa magari hayo linatokana na maswali ya dodoso aliyoulizwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala kwa shahidi namba 22, Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, SSP David Mhanaya, mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kutokana na ushahidi wake aliotoa mahakamani.

"Wakati unatoa ushahidi wako hapa, ulisema kulikuwa na ugomvi wa mali kati ya Mrita na marehemu Aneth na kitu ambacho kiliunganishwa katika mauaji hayo ni mteja wangu kuanza kuuza mali ikiwamo kubadilisha umiliki wa magari yote. Sasa ninataka ujibu maswali yangu," Kibatala alidai.

**Kibatala: Shahidi, hebu shika hii nyaraka ya Malamlaka ya Mapato (TRA) ambayo ilikwenda kwa huyo aliyekutuma kufanya kazi hii, wakimweleza hali ya magari kadha wa kadha. Nyaraka hiyo ambayo iliandikwa Julai 20, 2017 na TRA, ulishawahi kuiona au kukutana nayo?**

**Shahidi:** Mimi sikukutana nayo.

**Kibatala: Kwahiyo, hili gari ambalo unalisema kwamba mteja wangu (Mrita) alilibadilisha umiliki kwa kuangalia hiyo nyaraka inaonesha vipi?**

**Shahidi:** Tena sio hili Landcruser tu, magari yote yalibadilishwa.

**Kibatala: Kuna kitu chochote ambacho kinaeleza hayo?**

**Shahidi:** Kadi za magari zote zinajieleza kasoro gari aina ya Suzuki Vitara, ambalo hatukuona sababu ya kufanya uchunguzi.

**Kibatala: Kwa mujibu wa barua ya TRA kwenda kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), inaeleza gari namba T 677 DMM lilibadilishwa jina la umiliki kutoka kwa Samwel Muze kwenda kwa Miriam Steven Mrita Desemba 10, 2013.**



**Shahidi:** Mimi ninachofahamu magari yalibadilishwa.

**Kibatala: Unajua gari hili lilibadilishwa umiliki miaka mitatu iliyopita kabla ya mauji?**

**Shahidi:** Suala la mwaka mimi sijui.

**Kibatala: Wewe unajua lilisajiliwa lini?**

**Shahidi:** Ninaomba usiniite wewe.

**Kibatala: Tulia wewe, hakuna ugomvi wewe.**

**Shahidi:** Naomba usiniite wewe.

**Kibatala:** Mheshimiwa Jaji, ninaomba shahidi apewe sheria za kwenye kizimba.

**Jaji:** (akaingilia) Shahidi sikiliza maswali halafu ujibu.

**Shahidi:** Mheshimiwa Jaji, asiniite wewe kama mtu ambaye hana maana.

**Shahidi:** Kwa mujibu wa hii nyaraka, jina liliosajiliwa ni Miriam Mrita.

**Kibatala: Endelea kuishika hiyo nyaraka, gari hilo linaonesha lilisajiliwa Mei 15, 2017 kwa jina la Domac Safari Limited, unamfahamu?**

**Shahidi:** Sifahamu (huku akiendelea kusoma nyaraka kimyakimya).

**Kibatala: Upo tayari shahidi?**

**Shahidi:** Swali langu unalikumbuka?

**Kibatala: Desemba 15, 2010 gari hili lilikuwa na umiliki wa Michael Masawe, Novemba 16, 2011 lilibadilishwa umiliki kwenda Samwel Muze na Desemba 10, 2013 kwenda kwa Miriam Mrita.**

**Pia, Mei 15,2017 gari hilohilo lilibadilishwa umiliki tena kwenda kwa Kampuni ya Domac Safari Ltd.**

**Shahidi:** Mheshimiwa Jaji, kipindi chote hicho kulikuwa na kesi ya mirathi inayoendelea huko Moshi, ambayo ilikuwa ni ya marehemu Erasto Msuya, mume wa Miriam.

Sikutaka kuzungumzia hili, lakini kwa sababu wakili kanitaka nifike huko, nitafanya hivyo, akasababisha niikumbuke mengi.

**Kibatala: Unafahamu msimamizi wa mirathi?**

**Shahidi:** Ninafahamu, lakini sio kuuza.

**Kibatala: Kwa tarehe hizo, gari hilo lilibadilishwa umiliki, wakati mume wake bado yupo hai, unalijua hilo?**

**Shahidi:** Sijui.

**Kibatala: Ni wapi kwenye hiyo nyaraka ya TRA inaonesha gari hilo aina ya Landcruser liliwahi kumilikiwa na marehemu Erasto Msuya? Mwambie Jaji na Wazee wa Baraza.**

**Shahidi:** Mheshimiwa Jaji, hakuna sehemu inayoonesha Erasto Msuya alikuwa mmiliki, lakini tunaamini mali zote zinamilikiwa na wanaume.

**Kibatala: Hiyo ni sheria au ni utaratibu gani huo, askari mpelelezi SSP Mhanaya?**

**Shahidi:** Tunaongea kwa mazoea.

**Kibatala: Katika nyaraka hiyo ya TRA, gari aina ya Range Rover T 800 CKF hebu soma usajili wake.**

**Shahidi:** Gari aina ya Range Rover namba T 800 CKF, Mei 14, 2013 lilikuwa limesajiliwa kwa jina la God Mwanga Investment Ltd na Desemba 12, 2013 lilibadilishwa umiliki kwenda kwa Miriam Mrita, mshtakiwa wa kwanza.

**Kibatala: Ni lini gari hilo lilibadilishwa kuwa ni mali ya marehemu Erasto Msuya?**

**Shahidi:** Haijawahi, lakini tulitilia shaka kwenye tarehe za ubadilishaji wa umiliki wa magari haya kwa sababu zilikuwa zimefuatana.

**Kibatala: Ni kosa la jinai kubadilisha umiliki? Halafu hiyo ya God Mwanga Ltd unaifahamu?**

**Shahidi:** Sifahamu! Lakini, mtu anatakiwa kufuata utaratibu.

**Kibatala: Nenda kwenye 'item number tatu' (kipengele cha...), gari aina ya Ford Ranger majina ni ya nani yaliyosajiliwa hapo?**

**Shahidi:** Ni gari namba T 307 CBH aina ya Ford Ranger, Julai 4, 2012 ilisajiliwa kwa jina la Miriam Steven Mrita.

**Kibatala: Ni lini gari hilo lilikuwa linamilikiwa na Erasto Msuya?**

**Shahidi:** Hajawahi kuwa mmiliki, lakini nilingia shaka kutokana na tarehe za usajili kuwa zimefuatana katika magari yote na pia kulikuwa na mirathi inaendelea.

**Kibatala: 2012 kulikuwa na mirathi ya nani, kwa sababu marehemu alikuwa bado hajafariki? Ni kesi ipi ya mirathi unayoizungumzia?**

**Shahidi:** Mimi sifahamu!

**Kibatala: Nenda kwenye 'item' (kipengele) namba nne gari namba T 429 BYY aina Rangerover, ueleze mahakama kuhusu umiliki.**

**Shahidi:** Hili gari limesajiliwa kwa jina la Erasto Msuya Machi 2, 2012 na ndiyo mmiliki hadi sasa na gari hilo kwa mujibu wa Getruda, ndilo lilikuwa linatumiwa na Mrita.

**Kibatala: Hili limebadilishwa lini umiliki kwa sababu ulisema magari yote yamebadilishwa?**

**Shahidi:** Hili halijabadilishwa.

**Kibatala: Sasa mteja wangu alikuwa anajitwalia mali gani hadi mkahusisha na masuala ya mauaji? Haya, hii Suzuki Vitara ilishawahi kumilikiwa na Erasto Msuya?**

**Shahidi:** Hapana, hili gari lenye usajili wa namba T 620 CBB Suzuki Vitara lilisajiliwa Juni 26, 2012 kwa jina la Sunshine Express Ltd na Julai 5, 2012 lilibadilishwa kutoka kwa Tendaeli Mollel na Novemba 27, 2015 lilibadilishwa tena umiliki kwenda kwa Miriam Steven Mrita.

**Kibatala: Ni sahihi gari hili halijawahi kumilikiwa na marehemu Erasto Msuya?**

**Shahidi:** Si sahihi kwa jina, lakini mali zote zilikuwa kwenye umiliki wa Msuya na zote zimebadilishwa.

**Kibatala: Yaani shahidi unazungumza kama mtu wa mitaani, yaani mali zikiwa kwenye eneo... (akakatishwa na shahidi)**

**Shahidi:** Mheshimiwa Jaji, na yeye anazungumza kama mtu wa mtaani, haoni ambacho kipo mbele mtu amebadili magari yote haya kwa muda mfupi ndiyo maana tukachukua tukayafanyia kazi. Walikuwa wanaishi kama mke na mume. Kwanini magari yamebadilishwa umiliki?

Kesi hiyo imeahirishwa hadi leo kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya tuhuma za mauaji hayo ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kukiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.

## TANTRADE yatangaza fursa bidhaa tisa kwa masoko ya nje

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE) imetangaza fursa ya bidhaa tisa zinazohitajika katika masoko ya nje ambazo ni mbaazi, dengu, korosho, kahawa, pamba, dhahabu, almasi, ufuta na vifungashio vya mifuko.

Pia inategemea kufumua Viwanja vya Maonyesho ya Sabasaba ili kujenga majengo yenye hadhi ya kimataifa ya maonyesho.

Mkurugenzi Mkuu Tantrade, Latifa Khamis, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na wahariri na waandishi wa habari, kueleza utekelezaji wa majukumu ya mamlaka hiyo.

Alisema fursa ya mauzo ya bidhaa hizo ni dola za Marekani milioni 5.25 na kwamba dhahabu ndiyo yenye fursa kubwa ikifuatiwa na korosho na ufuta.

Alisema bidhaa hizo zinazohitajika katika nchi za India, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uswisi, Vietnam, China, Pakistani, Japan, Marekani, Oman, Qatar, Kuwait na Saudi Arabia.

"TANTRADE imekamilisha maombi ya ufadhili ya kuendeleza rajamu (branding) ya taifa ya viungo na kwa sasa tumeshakamilisha rajamu ya iliki, tangawizi, mdalasini, pilipili manga na karafuu. Mamlaka inaendelea na taratibu za kukamilisha rajamu za bidhaa za asali, korosho, kahawa na chai," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mamlaka hiyo imetoa mafunzo kwa wafanyabiashara 6,979 ili kuwajengea uwezo wa kujiendesha kiushindani.

Alifafanua kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, TANTRADE ilifanikiwa kuratibu matukio yaliyowawezesha mikataba na makubaliano 46 ya kibiashara kusainiwa yenye thamani ya Sh. trilioni 17.53.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi huyo ameonya watu wanaoandaa maonyesho na misafara ya kibiashara bila kufuata utaratibu na kwamba kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

Latifa aliwataka wananchi kuepuka kutapeliwa kwa kushiriki misafara hiyo bila kujiridhisha kama kampuni inayotangaza fursa husika ina sifa ya kufanya kazi hiyo.

Kuhusu mapato ya TANTRADE, Latifa alisema katika kipindi cha miaka mitano, mamlaka hiyo ilipanga kukusanya Sh. bilioni 52.5, lakini ilikusanya Sh. bilioni 40 sawa na asilimia 76 ya lengo. Mwaka jana ilitoa gawio la Sh. milioni 257 kwenye mfuko mkuu wa serikali.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa hivi sasa mamlaka inajiandaa kushiriki maonyesho makubwa ya kimataifa ya Expo 2025 yatakayofanyika jijini Osaka, Japan na kuzitaka taasisi kuchangamkia fursa zinazotokana na tukio hilo.

## ZISIKUPITE

### RAMOS HUYOOO SEVILLA

NAHODHA wa zamani wa Hispania, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 37, amepiga hatua katika mazungumzo ya kurejea kwake Sevilla miaka 18 baada ya kuondoka katika klabu hiyo na kujiunga na Real Madrid. Beki huyo aliondoka Paris St-Germain msimu huu wa majira ya joto wakati mkataba wake ulipomalizika. ***(ESPN)***

### PALHINHA NA BAYERN

KAKA yake Joao Palhinha amesema uhamisho wa kiungo wa Ureno na Fulham kwenda Bayern Munich "uliahirishwa", baada ya mazungumzo kuvunjika siku ya mwisho ya uhamisho wa wachezaji. ***(Mail)***

### MADDISON AANIKWA CHELSEA

CHELSEA ilitoa nafasi kwa Tottenham kumsajili kiungo wa kati wa England, James Maddison mwenye umri wa miaka 26, msimu wa majira ya joto kwa sababu hakuendana na wasifu wa umri wa walengwa wao wa uhamisho. ***(Football Insider)***

### DE GEA ATAKIWA SAUDIA

GOLIKIPA wa zamani wa Manchester United na Hispania, David de Gea mwenye umri wa miaka 32, ni miongoni mwa wachezaji kadhaa wanaopatikana kwa uhamisho wa bure ambao unavutia klabu za Saudia. ***(Marca)***

### ATAJWA SAUDIA

WINGA wa Atletico Madrid na Ubelgiji, Yannick Carrasco mwenye umri wa miaka 29, anatazamiwa kuhamia Al Shabab ya Saudia kwa pauni milioni 12.8. ***(ESPN)***

### ROONEY KUKOSA NYOTA

MATUMAINI ya kocha Wayne Rooney kuwasajili tena kiungo wa Jamaica, Ravel Morrison mwenye umri wa miaka 30, kiungo wa kati wa England, Jesse Lingard mwenye miaka 30, na mshambuliaji wa Ghana, Andre Ayew (33), ambapo wote ni wachezaji huru, yamezimwa na masuala ya mishahara katika Klabu ya MLS DC United. ***(Washington Post)***

### ADARABIOYO AWANIWA

KLABU ya Monaco ya Ligue 1 inapanga kumsajili beki wa Fulham, Tosin Adarabioyo mwenye umri wa miaka 25 katika dirisha la Januari baada ya kujitahidi sana kufanikisha dili lake katika uhamisho wa msimu wa majira ya joto. ***(Fabrizio Romano)***

### BARCA HAIJAFURAHISHWA

BARCELONA haijafurahishwa na majaribio ya Manchester City kumsajili beki wa kushoto na Hispania, Alejandro Balde, 19. ***(Mundo Deportivo)***

### SILVA, MASHABIKI WAZOZANA

MLINZI wa Chelsea na Brazil, Thiago Silva mwenye umri wa miaka 38, alizozana na mashabiki kwenye Instagram baada ya klabu hiyo kufungwa na Nottingham Forest katika mechi ya Ligi Kuu England, Jumamosi. ***(Telegraph)***

### MATA ATUA KOBE

NI rasmi Juan Mata ametua Vissel Kobe baada ya kuondoka Galatasaray. Mata amejiunga na klabu hiyo ya Japan ambayo nguli wa Hispania na Barcelona, Andrés Iniesta, aliichezea kwa miaka 5. ***(Marca)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RICE NI SHUJAA MPYA WA ARSENAL - NEVILLE

**LONDON,** England

**Amekuja katika klabu hii ya soka kuwa mleta tofauti, anawasalimu watu...**

GARY Neville amemsifu 'mtengeneza tofauti', Declan Rice, huku kiungo huyo wa Arsenal akifunga bao lake la kwanza kwa klabu hiyo katika ushindi wa mabao 3-1 walioupata 'Washikabunduki' hao dhidi ya Manchester United, Jumapili.

**Ilionekana kuwa wapinzani hao wawili wa zamani walikuwa wakielekea kugawana pointi wakati mchezo ulipoingia dakika nane za nyongeza wakiwa wamefungana bao 1-1 kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.**

Lakini Rice alipata nafasi upande wa kushoto wa kisanduku kutoka kona ya Arsenal na kumfyatua Andre Onana kupitia kwa mpira uliomgonga Jonny Evans na kuwapa bao la pili vijana wa Mikel Arteta.

Akichambua mchezo kupitia Sky Sports, Neville alizungumzia bao la Rice na kudai ni wakati kama huu ndio uliowafanya Washikabunduki hao kuvunja benki na kutoa kitita cha rekodi kwa ajili ya kiungo huyo wa kati wa England.

"Declan Rice amekuja katika klabu hii ya soka kuwa mleta tofauti," alisema Neville. "Anawasalimu watu wanaomuamini mbele yake. Mashabiki wa Arsenal wanampenda, wamepata shujaa mpya na amecheza mechi chache tu.

"Ndio maana alikuja hapa, ndio maana walilipa fedha nyingi. Dakika kubwa, mechi kubwa."

Rice alifanya mashabiki kulipuka kwa shangwe kwenye dimba la Emirates huku akizongwa na wachezaji wenzake na kuwakimbilia mashabiki kushangilia bao la dakika za lala salama.

Furaha hiyo haikuishia hapo, kwani Gabriel Jesus aliongeza bao la tatu dakika ya 98 na kuipa Arsenal uhakika wa pointi zote tatu.

Hapo awali, Marcus Rashford alikuwa ameiweka Man United uongozini na kuanza mchezo huo kwa kasi.

Lakini Arsenal walipata bao ndani ya dakika moja kupitia kwa Martin Odegaard na kusawazisha bao hilo.

Kikosi cha Erik ten Hag kilifikiri kuwa kimeshinda mchezo huo wakati Alejandro Garnacho alipokimbia na kuuweka mpira wavuni, lakini VAR ikalikataa bao hilo kwani ilionesha kuwa alikuwa ameotea.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
BARNSLEY
VERSUS
GRIMSBY
1 | 1.79
X | 3.57
2 | 3.82

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SANCHO ALIA TEN HAG KUMFANYA MBUZI WA KAFARA



**MANCHESTER,** England

JADON Sancho amejibu madai ya Kocha wa Manchester United, Erik Ten Hag, kwamba aliondolewa katika kikosi kilichofungwa na Arsenal kwenye Ligi Kuu England kwa kuwa duni mazoezini, akisema "nimefanywa kuwa mbuzi wa kafara."

Sancho mwenye umri wa miaka 23, aliachwa nje ya kikosi cha siku ya mechi kwa ajili ya safari ya Emirates, ambayo United ilifungwa mabao 3-1, na Ten Hag alisema baada ya mchezo huo kuwa winga huyo ameshindwa kufikia viwango vya mazoezi wiki hii.

"Katika uchezaji wake kwenye mazoezi hatukumchagua," alisema Ten Hag alipoulizwa kuhusu kukosekana kwa Sancho kwenye kikosi.

"Lazima ufikie kiwango kila siku ndani ya Manchester United. Unaweza kufanya uchaguzi katika mstari wa mbele, kwa hiyo katika mchezo huu hakuchaguliwa."

Lakini ndani ya saa moja ya maoni ya Ten Hag katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi, Sancho alitoa taarifa kupitia mtandao wa X (zamani Twitter) akikanusha madai hayo akisema "si ya kweli kabisa."

"Tafadhali usiamini kila kitu unachosoma! Sitaruhusu watu kusema mambo ambayo si kweli kabisa," aliandika Sancho.

"Nimejiendesha vizuri katika mazoezi wiki hii.



## Sergio Ramos arejea tena Sevill

**SEVILLE,** Hispania

SERGIO Ramos yuko kwenye hatua za mwisho kabisa kurejea Sevilla, kwa mujibu wa ESPN.

Ramos mwenye umri wa miaka 37, amekuwa mchezaji huru tangu mkataba wake na Paris Saint-Germain ulipomalizika Julai mwaka huu.

Beki huyo wa kati wa zamani wa Real Madrid alizivutia Klabu za Al Ittihad ya Saudi Arabia, Galatasaray, FC Porto na Ligi Kuu ya Marekani (MLS), vyanzo vilisema, lakini amechagua Sevilla kwa kuwa anapendelea kukaa karibu na nyumbani.

Sevilla ambao mchezo wao wa LaLiga huko Atletico Madrid uliahirishwa Jumapili kwa ushauri wa viongozi wa eneo hilo, kwa sababu ya utabiri wa mvua kubwa - wanatarajia kukamilisha dili hilo saa chache zijazo.

Rais wa klabu, Pepe Castro alionekana kukataa mpango wa kumnunua Ramos mwezi uliopita, akisema "hajawahi kuwa chaguo" na akas beki huyo alipewa k "moja kwa moja na kwa isiyo ya moja kwa moja."

Sevilla - walioshinda ya Europa Mei mwaka wamekuwa na mwa mbaya msimu huu wa La wamepoteza mechi zote hadi sasa na wako mk mwa msimamo.

Ramos alizaliwa Camas ulio nje kidogo ya Jiji la Se na aliichezea Sevilla ak kijana kabla ya kujiunga Real Madrid Septemba 2

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA



# UKARABATI UWANJA WA MKAPA KUKAMILIKA KABLA UFUNGUZI AFL

**Na Shufaa Lyimo**

UKARABATI wa Uwanja wa Benjamin Mkapa, unaendelea kupamba moto baada ya serikali kuanza kwa kasi kutekeleza agizo la Shirikisho la Soka duniani (FIFA) na la Afrika (CAF), kuelekea michuano ya African Football League (AFL), ambayo ufunguzi wake utafanyika uwanjani hapo Oktoba 20, mwaka huu.

Michuano hiyo inayoshirikisha klabu nane bora barani Afrika, Simba ni timu pekee katika Ukanda wa Afrika Mashariki (Cecafa), itakayoshiriki, ambapo pia itafungua kitimtim hicho katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Al Ahly ya Misiri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Uwanja huo, Paul Mahona, alisema kuhakikisha baadhi ya maeneo yamekamilika hadi ifikapo Oktoba 20, mwaka huu ili ufunguzi huo ufanyike uwanjani hapo kama ilivyopangwa.

"Tunakimbizana na muda kuhakikisha siku chache zilizobaki tunazitumia vizuri ili ifikapo Oktoba 20, mwaka huu baadhi ya maeneo yawe yamekamilika ambapo Simba itaanza mchezo wake (dhidi ya Al Ahly)," alisema Mahona.

Meneja huyo alisema hadi kufikia tarehe hiyo, marekebisho ya awali yatakuwa yamekamilika na kwamba baadhi ya vitu vya zamani vilivyokuwa ndani ya uwanja huo tayari vimetolewa.

"Mkandarasi anaendelea kuyafanyia kazi maeneo hayo ikiwamo vyumba vya wachezaji tayari makabati yametolewa vilevile eneo la waandishi wa habari viti vilivyokuwapo vimetolewa, tunaamini uwanja huu utakuwa bora," alisema meneja huyo.

Alisema maboresho hayo yatachukua muda mrefu kutokana kwamba kila eneo litaguswa na kuweka wazi kuwa wameimarisha usalama.



Mafundi ujenzi wakiendelea kupaka rangi Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

## Simba kuigeuza Power Dynamos daraja la Al Ahly

INATOKA UKURASA 24

na Power Dynamos kusaka ushindi kwa michezo yote miwili na kutinga hatua ya makundi lakini pia kuitumia kama sehemu ya maandalizi dhidi ya Al Ahly.

"Tunatambua ugumu wa michuano iliyopo mbele yetu na ninaamini Robertinho anaendelea na maandalizi kufikia malengo yetu, kushinda kila mechi iliyopo mbele yetu, hatutaki kwenda kushiriki, tunataka kuwa miongoni mwa timu zinazokwenda kushindana na klabu kubwa ikiwamo Al Ahly na zitakazokuwa mbele yetu," alisema mwenyekiti huyo.

## *Maxi ashtua 'mavitu' ya Gamondi kwa Al-Merrikh CAF*

INATOKA UKURASA 24

unatumia saa tatu, faida nyingine ni kwamba hii ni Afrika Mashariki, hivyo tuna mashabiki wetu ukanda huu ikiwamo Rwanda, tunawakuta mashabiki wetu huko, kuna mikoa ya karibu kama vile Kigoma, Mwanza na Kagera, najua mashabiki wengi watamiminika kwenda kuishangilia Yanga na kuwapa sapoti wachezaji wetu wajione kama wako nchini Tanzania," alisema Kamwe.

Alisema kwa mazingira yaliyopo anaona kabisa ni kama Yanga inacheza mechi yake hiyo ya ugenini ikiwa nyumbani.

"Kwa maana hiyo tunataka kuimaliza kabisa mechi katika pambano hilo la kwanza ili tukirejea nchini kazi yetu iwe moja tu, kucheza na mahesabu kwa ajili ya kutinga hatua ya makundi," alisema.

Kamwe alisema kwa siku hizi mbili watatoa utaratibu wa mashabiki wa Dar es Salaam jinsi gani ya kufanya ili kusafiri mpaka Kigali nchini Rwanda kwa ajili ya mechi hiyo.



## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 05/09/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 17:00 | 5971 | Al-Arabi vs Buqaa Amman | 2.00 | 3.20 | 3.46 |
| 18:00 | 1252 | Admira Prague vs Baumit Jablonec | 9.01 | 5.94 | 1.22 |
| 18:00 | 1945 | Goerslev IF vs Ishoej IF | 3.93 | 3.93 | 1.69 |
| 18:00 | 3682 | Taastrup FC vs FA 2000 | 18.27 | 9.34 | 1.07 |
| 18:00 | 5278 | Birkerod Skjold vs Vanloese | 18.27 | 9.34 | 1.07 |
| 18:00 | 5474 | Oureskolernes BK vs AB Gladsaxe | 3.45 | 3.75 | 1.78 |
| 19:30 | 2563 | Bronshoj BK vs B 93 Copenhagen | 5.40 | 4.20 | 1.44 |
| 20:00 | 1524 | SC Eltersdorf vs VfB Eichstatt | 1.71 | 3.86 | 3.91 |
| 20:00 | 1854 | B 1908 Amager vs HIK Hellerup | 5.40 | 4.20 | 1.43 |
| 20:00 | 2180 | Skive IK vs Thisted FC | 2.26 | 3.50 | 2.55 |
| 20:00 | 5562 | Grorud IL 2 vs Gjellerasen | 5.65 | 5.65 | 1.32 |
| 20:30 | 4501 | SG Aumund-Vegesack vs FC Oberneuland | 1.50 | 4.77 | 4.46 |
| 21:00 | 1208 | AFC Wimbledon vs Stevenage | 2.66 | 3.32 | 2.37 |
| 21:00 | 2137 | Forest Green vs Shrewsbury | 2.46 | 3.25 | 2.59 |
| 21:00 | 2918 | Northampton vs Oxford Utd | 2.80 | 3.21 | 2.31 |
| 21:00 | 3222 | CA Platense vs Defensores de Belgrano | 1.19 | 5.40 | 11.00 |
| 21:00 | 5032 | Barrow vs Blackpool | 2.74 | 3.35 | 2.29 |
| 21:00 | 5417 | Fleetwood Town vs Tranmere | 1.92 | 3.45 | 3.45 |
| 21:00 | 5654 | Gillingham vs Leyton Orient | 2.21 | 3.31 | 2.90 |
| 21:30 | 2172 | Deportivo Riestra vs Chacarita Juniors | 2.70 | 2.95 | 2.56 |
| 21:30 | 2752 | Barnsley vs Grimsby | 1.79 | 3.57 | 3.82 |
| 21:30 | 4201 | Leandro N Alem vs General Lamadrid | 2.94 | 2.94 | 2.38 |
| 21:45 | 1240 | Crawley Town vs Charlton | 2.75 | 3.36 | 2.28 |
| 21:45 | 1508 | Chester vs Hereford United | 1.79 | 3.41 | 4.02 |
| 21:45 | 1641 | Worthing vs Welling | 1.48 | 4.20 | 5.32 |
| 21:45 | 1710 | Bolton vs Salford City | 1.62 | 3.83 | 4.49 |
| 21:45 | 1848 | Ayr United vs Falkirk FC | 1.80 | 3.60 | 3.50 |
| 21:45 | 2612 | Banbury United vs Alfreton | 2.75 | 3.26 | 2.33 |
| 21:45 | 2654 | Peterborough Sports vs Curzon | 2.55 | 3.26 | 2.50 |
| 21:45 | 2820 | Southport vs Scarborough Athletic | 3.12 | 3.48 | 2.03 |
| 21:45 | 3089 | Maidstone vs Aveley FC | 2.27 | 3.31 | 2.80 |
| 21:45 | 3124 | Darlington vs Boston Utd | 2.65 | 3.37 | 2.35 |
| 21:45 | 3142 | Truro City vs Bath City | 2.15 | 3.37 | 2.96 |
| 21:45 | 3310 | Gloucester City vs Buxton FC | 2.90 | 3.41 | 2.16 |
| 21:45 | 3375 | Tonbridge Angels vs Braintree | 2.08 | 3.42 | 3.06 |
| 21:45 | 3577 | St.Albans vs Dover | 1.73 | 3.56 | 4.17 |
| 21:45 | 3579 | Tamworth vs Chorley | 2.30 | 3.25 | 2.80 |
| 21:45 | 3747 | Bishop Stortford vs Rushall Olympic | 2.08 | 3.36 | 3.11 |
| 21:45 | 3839 | Kings Lynn vs Brackley Town | 2.69 | 3.20 | 2.40 |
| 21:45 | 3845 | Scunthorpe vs South Shields | 1.84 | 3.52 | 3.68 |
| 21:45 | 4113 | Bristol Rovers vs Cheltenham | 1.78 | 3.55 | 3.91 |
| 21:45 | 4121 | Warrington Town vs Spennymoor Town | 2.69 | 3.41 | 2.30 |
| 21:45 | 4163 | Port Vale vs Crewe | 1.70 | 3.73 | 4.08 |
| 21:45 | 4341 | Hanwell Town vs Chesham Utd | 3.36 | 3.77 | 1.86 |
| 21:45 | 4469 | Accrington vs Carlisle | 2.33 | 3.35 | 2.69 |
| 21:45 | 4493 | Dartford vs Slough Town | 1.86 | 3.61 | 3.51 |
| 21:45 | 4752 | Weston Super Mare vs Yeovil | 3.05 | 3.41 | 2.09 |
| 21:45 | 4948 | Torquay vs Farnborough Town | 2.06 | 3.35 | 3.15 |
| 21:45 | 5075 | Hampton and Richmond vs Weymouth | 2.11 | 3.41 | 3.00 |
| 21:45 | 5231 | Blyth Spartans vs Farsley Celtic | 2.00 | 3.41 | 3.25 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumanne Septemba 5, 2023

Nipashe



Ramos arejea tena Sevilla UKURASA 22

# Maxi ashtua 'mavitu' ya Gamondi kwa Al-Merrikh

## ●●● Aiona Yanga makundi, wakunwa kupelekwa Uwanja wa Pele Rwanda huku...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI kiungo mshambuliaji wa Yanga, Maxi Mpia Nzengeli, akisema kutokana na program wanayopewa na Kocha Miguel Angel Gamondi, ni suala la muda tu kukata kiu ya mashabiki wao kuona timu yao ikicheza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, uongozi wa klabu hiyo umeeleza kufurahishwa na mchezo wao dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan kuchezwa nchini Rwanda katika Uwanja wa Pele, Nyamirambo.

**Yanga ili wafanikiwe kutinga katika hatua ya makundi ya michuano hiyo ambayo wameikosa kwa miaka 24 sasa, wanatakiwa kuhakikisha wanapata matokeo ya jumla dhidi ya Al-Merrikh, wakianza na mchezo wa Septemba 16, mwaka huu kabla ya kurudiana nchini Septemba 29, mwaka huu.**

Akizungumza na Nipashe jana, Max alisema malengo yake ni kuhakikisha anaisaidia timu hiyo kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa na kufikia malengo yao ya kutinga hatua ya makundi.

"Malengo ya timu ndio ya wachezaji wote, kwetu tunatamani kuona tunafika makundi na kupita zaidi ya hapo, kikubwa tunachokifanya kwa sasa ni kuona tunapambana zaidi kwenye michezo yetu.

"Kocha anaendelea kufanya majukumu yake hasa kufanyia kazi makosa aliyoyaona kwenye mechi zilizopita, kuhakikisha tutashinda michezo yetu miwili iliyo mbele yetu dhidi ya Al Merrikh," alisema Nzengeli.

Alisema muhimu zaidi kwa upande wao ni kuona wanafanya vizuri na kupata matokeo, tuna uwezo huo na tutapambana zaidi kufikia malengo yetu.

Nzengeli alisema anaimani na timu yao kufanya vizuri katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kiu yake ni kuona kwanza Yanga ikitinga hatua ya makundi kwa mara ya kwanza baada ya miaka kadhaa.

Katika hatua nyingine uongozi wa klabu hiyo umesema umefurahi Al-Merrikh kupanga mchezo wao wa raundi ya kwanza kuchezwa Rwanda katika Uwanja wa Pele, Nyamirambo uliopo jijini Kigali.

Yanga ambayo itakipiga mechi yake ya raundi ya kwanza Septemba 16 nchini humo badala ya Sudan ambapo kuna machafuko ya kisiasa, imesema kucheza kwao mechi nchini Rwanda kuna faida nyingi zaidi kuliko wapinzani wao, hivyo wanaona ni fursa ya kupata ushindi ugenini kabla ya kumalizia nyumbani.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema jana kuwa watatumia faida hiyo kukusanya mashabiki kwenye mikoa jirani kama Kagera, Mwanza na hata Kigoma kwa ajili ya kwenda kuwashangilia.

"Kusema kweli kuchezea nchini Rwanda ni faida kubwa kwetu kuliko hasara, kwani ni karibu kuliko tungekwenda kucheza Sudan, au Morocco walikotaka kutupeleka, kule Kigali kwa ndege

INAENDELEA UKURASA 23



Maxi Nzengeli

## Simba kuigeuza Power Dynamos daraja la Al Ahly

**Na Saada Akida**

HUKU kikosi chao kikiendelea na maandalizi makali kuelekea mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia, uongozi wa klabu hiyo umesema watatumia michezo yao miwili dhidi ya Wazambia hao kujiandaa dhidi ya Al Ahly kwenye mechi ya African Football League, AFL.

Simba ambayo Septemba 16, itakuwa ugenini nchini Zambia kucheza mechi hiyo ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kurudiana Septemba 29 hapa nchini, ndiyo itakayocheza mechi ya ufunguzi ya michuano ya African Football League katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Al Ahly.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again', akizungumza na Nipashe, amesema baada ya kujua wapinzani wao wa Raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika ni Power Dynamos ya Zambia pamoja na Al Ahly katika michuano ya Afrika Football League, Kocha Roberto Oliveira anafanya maandalizi makali.

Try Again alisema dhamira yao ni kushinda mataji ya ndani na kufika hatua ya nusu fainali ya Afrika pamoja na kushindana katika michuano mikubwa ya AFL.

Alisema benchi la ufundi linaloongozwa na Robertinho, linafanya kazi yake kwa umakini baada ya kumpatia kila kitu ikiwamo usajili wa wachezaji wenye uwezo na uzoefu mkubwa wa michuano ya Afrika.

"Tumefanya usajili mkubwa sana kupitia dirisha kubwa la usajili mwaka huu na ukweli ni kuwa miongoni mwa sababu kubwa ni ushiriki wetu wa mashindano mbalimbali ikiwamo ya AFL, tumejipanga kushindana katika michuano yote mikubwa kufikia malengo yetu," alisema Try Again.

Aliongeza kuwa wanauzoefu mkubwa wa mashindano ya kimataifa, wanaenda kucheza

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042